

MUHURI WA TANO



Tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi.

² Baba yetu wa Mbinguni mwenye rehema, Mungu Mwenyezi, Ambaye ulimfufua Yesu Kristo tena kutoka kwa wafu, Na umemleta kwetu katika siku hizi za mwisho, katika Nguvu za Roho Mtakatifu, tunashukuru kwa ajili ya kujiliwa huku kukuu kwa Mungu asiyeweza kuona uharibifu. Na sasa, Baba, tunaikabili saa nyingine, saa ambayo huenda ikabadilisha kikomo cha Milele cha watu wengi.

³ Na kuendea jambo hili, Bwana, sisi hatustahili. Kwa sababu, liko kwenye Maandiko, ya kwamba, “Mwana-Kondoo alikichukua kile Kitabu na kuifungua ile Mihuri.”

⁴ Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, njoo, tunaomba. Tunakuita Wewe, Bwana, Mkombozi aliye mkuu. Njoo na utuonyeshe mpango Wako wa ukombozi ambao umefichwa kwa miaka yote, ukituvunjia Muhuri huu wa Tano usiku wa leo, Baba, na kutufunulia kilicho chini ya Muhuri huo; ili kwamba tuondoke twende tukiwa Wakristo bora zaidi kuliko tulivyo sasa, tuweze kustahili vizuri zaidi kwa kazi iliyo mbele. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

Ketini.

⁵ Habari za jioni, marafiki. Ninahesabu haya kwamba ni majaliwa mazuri sana kuwapo hapa usiku wa leo, kwenye tukio hili kuu. Sijui mahali po pote ambapo ningeweza kujisikia vizuri zaidi kuwako hapo, kuliko kuwa kazini mwa Mfalme. Na sasa tukija maalumu kwa ajili ya masomo haya ambapo tunangojea tu; kama Yeye hangenifunulia Hayo, nisingeweza kuwapa ninyi Hayo. Sijaribu kutumia mawazo yangu yo yote wala cho chote kile; ni vile tu atakavyonipa Hayo. Hiyo ni kweli. Nami ni—nina hakika, kama situmii mawazo yangu mwenyewe, Nalo lije jinsi vile limekuja. Na kote maishani halijakosea kamwe. Halitakosea wakati huu.

⁶ Sasa, sasa tunafurahi kwa furaha kuu sana na tunashukuru sana sana, kwa ajili ya yale aliyotufanyia, ule mkono mkuu wa siri wa Mungu aliye hai! Ni jambo gani kubwa zaidi lingaliweza kuwa, tungeweza kuwa watu waliobarikiwa zaidi kiasi gani, kuliko kuwako mbele yetu kwa Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana?

⁷ Labda tungepuliza filimbi na—na kupandisha bendera, na kutandaza mazulia na kila kitu, kwa ajili ya Rais wa taifa hili kuja kwenye jiji hili. Lakini, hebu wazienu tu, jambo hilo lingekuwa ni sawa, na ingekuwa ni heshima kwa mji huu.

⁸ Lakini wazia. Katika maskani yetu ndogo, nyenyekevu, usiku wa leo, tunamwalika Mfalme wa wafalme, Mungu. Nasi hatuninii. . . Yeye hahitaji kutandaziwa mazulia huko nje, na kadhalika. Yeye anatamani mioyo minyenyekevu itandazwe, ili kwamba aweze kuichukua mioyo hii minyenyekevu na kuifunulia ma—mambo mema aliyoyaweka akiba kwa ajili ya wote wampendao.

⁹ Sasa, tuliuliza. . . Nami nina ushuhuda ambao ningetaka ku—kuutoa. Sasa, kama nimekosea juu ya jambo hili; mimi nimelisikia tu sasa hivi, na ningeweza kuwa nimekosea. Lakini nadhani watu hao wako hapa, na ambao ushuhuda huo unawahusu.

¹⁰ Na halafu, siku chache zilizopita, wakati nilipokuwa nimeenda nyumbani kwangu sasa, kule—kule Arizona, tulipata wi—wito uliosema kulikuwa na mvulana mdogo aliyekuwa na ugonjwa wa homa ya baridi yabisi. Na huo huenda kwenye moyo. Naye alikuwa ninii sana. . . Baba yake na mama yake ni marafiki wangu wependwa sana na wa thamani. Ilikuwa ni mmoja wa mashemasi wetu hapa, wa kanisa, Ndugu Collins. Mvulana wake mdogo, Mikey kadogoo, anayecheza na Joe, alikuwa akiugua homa ya baridi yabisi ya moyo. Na madaktari walikuwa wamemrudisha nyumbani, wakamlaza kitandani, na wakawaambia wazazi wake hata wasimwache aamke, wala kuinua kichwa chake, kunywa maji. Ayanywe kwa mrija; alikuwa na hali mbaya sana. Nao wazazi, ni waaminifu, wanahudhuria maskani hii hapa, na wanaamini.

¹¹ Na siku chache zilizopita usiku, bila kujaribu kungojea, tulitangaza ibada za kuponya Jumapili. Lakini, kuona kwamba tulikuwa tujibu maswali, kwa hiyo basi ilitubidi kuondoa ibada ya ponyaji.

¹² Na halafu mimi nilikuwa na jambo fulani dogo nililokuwa nimeliweka ndani yangu, moyoni mwangu.

¹³ Na mama wa yule mtoto na baba walitaka kujua kama wangeweza kumleta mtoto huyo chu—chumbani. Ndipo wakamleta humo yule kijana mdogo, naye Roho Mtakatifu akamtangaza kwamba amepona.

¹⁴ Na kwa hiyo, wazazi wake, wakiwa wanaheshimu jambo hilo, walimrudisha mtoto huyo mdogo yumbani na kumpeleka shuleni, wakampeleka tu shuleni.

¹⁵ Daktari akapata habari, basi daktari hakufurahia sana jambo kama hilo. Kwa hiyo, akamwambia mama yake ya kwamba mtoto huyo anapaswa kuwa kitandani, lazima. Naye mama akamsimulia hadithi hiyo. Na ninafikiri mtu huyo ni, nasikia, Mkristo mwamini, wa madhehebu. M—Msabato, huyo daktari. Na kwa hiyo akasema, “Vema, mlipaswa. . . wakati wa huyo mtoto umefika, nipate kumchunguza.” Kasema, “Mnapaswa, angaa, kumwacha achunguzwe kwanza.”

Akasema, “Vema kabisa.”

¹⁶ Akampeleka mtoto kule, naye daktari akamfanyia uchunguzi, wa damu, mahali ambapo homa ya baridi yabisi huwa. Na kwa hiyo ninasikia ya kwamba huyo daktari alishangaa sana hakujuua la kufanya. Mvulana mdogo huyo ni mzima kabisa, ana afya na amepona, hamna hata ninii...?... ilionekana.

¹⁷ Sasa, je! akina Collins wako hapa? Huenda nimesimulia tukio hilo makosa. Ninataka...Hiyo ni kweli, Dada Collins? Naam. Vema. Naam. Huyo ni mtoto Mikey Collins, ana umri wa kama miaka sita, saba.

¹⁸ Na hilo lilitukia mle chumbani, yapata siku tatu usiku zilizopita. Loo! wao...Ilibidi pawe na Mtu fulani mle chumbani mbali na mwanadamu! Ilikuwa ni—ni Yehova aliye mkuu na mwenyezi, hiyo ni kweli, anayekuja kuheshimu Neno Lake. Nami nina—ninashukuru sana kusikia jambo hilo. Unaona? Najua sote tunashukuru. Si mimi tu, bali sisi sote tunashukuru, kwa sababu vipi kama huyo angekuwa—angekuwa ni mvulana wako mdogo ama ni mvulana wangu mdogo?

¹⁹ Na, kumbukeni, ninatoa ushuhuda, kama mmoja tu, na kuchukua mmoja hapa na pale. Inatendeka kila mahali, lakini ili kuwajulisha tu ya kwamba—ya kwamba huduma yangu halisi ni ya uponyaji wa Kiungu. Lakini wewe...Niko hapa kwa ajili ya Mihuri hii. Kwa sababu, baadaye kidogo, mtafahamu ni kwa nini ilinibidi kufanya jambo hili. Na, kwa hiyo, mimi si mwalimu, mimi si mwanatheolojia. Mimi—mimi huombea tu wagonjwa, na ninampenda Bwana. Na sasa, sasa katika jambo hili, ingawa, kwamba... .

²⁰ Jana usiku tulitoa ushuhuda wa yule msichana mdogo... Nina jina lake. Na Billy analo hapa sasa, mahali fulani, la huyo mzazi wake, na kwamba wao ni nani. Na msichana huyu mdogo alikuwa katika hatua ya mwisho ya lukemia, karibu tu...Alikuwa mgonjwa sana hata hawakuweza kumlisha kwa mdomo huu tena; ilibidi afanyiwe hivyo...aliweke damu kupitia kwenye mishipa. Naye alikuwa maskini mtoto mdogo mwenye sura nzuri. Alikuwa ni mdogo kwa umri wake, karibu kama huyu msichana mdogo hapa, nadhani. Lakini alikuwa mrefu kiasi *hiki*, ninii sana...Wao walikuwa kama wengi wetu. Ungeweza kutambua kwa nguo alizovaa mtoto huyo, ya kwamba...na wazazi wake, ya kwamba walikuwa ni maskini sana, fukara kabisa, na, kwa hiyo, bali walikuwa na uchaji sana. Ndipo Roho Mtakatifu akamtamkia mtoto huyo kwamba amepona.

²¹ Sasa, wazia tu jambo hilo, akiwa na lukemia, mtoto huyo mdogo. Na damu yake ilikuwa mbaya sana hata wasingeweza kumlisha kwa mdomo tena. Ilibidi wachukue, waende hospitali na wachukue damu, ama kuwekewa damu kupitia kwenye

mishipa, wamlishe; nadhani, glukosi, ama cho chote kile. Sijui wanatumia lugha gani ya kiganga kwa ugonjwa huo, lakini, hata hivyo, ilibidi alishwe kwa namna hiyo. Na kabla mtoto huyo hajaondoka mahali pale, alililia sambusa.

²² Na hao wazazi, baada ya wao kumsikia Roho Mtakatifu, juu ya BWANA ASEMA HIVI, unaona, wao...Na, wao, ni wageni, hawajawahi kamwe kufika pale. Lakini wao... Maskini mke na mume wa—wazuri sana ambao waliwapatia viti hapa, dakika chache zilizopita, Ndugu na Dada Kidd, walikuwa wamewaelekeza juu ya wanayopaswa kufanya, na yale wangesikiliza. Na mtoto huyo alikula chakula chake walipokuwa wanaenda zao nyumbani.

²³ Siku mbili ama tatu baadaye, alikuwa shuleni. Naye alibidi aende kwa daktari, na daktari alishangaa sana! Akasema, “Hakuna hata dalili moja ya leukemia inayoonekana kwa mtoto huyu.” Unaona? Sasa, hilo ni la pale pale, kwenye alama kabisa, Nguvu za Mwenyezi Mungu, kuchukua damu inayozunguka mwilini na kuisafisha kabisa, moja kwa moja namna hiyo, na—na kuweka kupigapiga kwa—kwa uzima mpya tena mle ndani. Maana, da—damu yako mwilini ndiyo uhai wako, wa kibinadamu. Na kuumba seli mpya, na kusafisha zile za zamani! Na—na hilo ni kwamba, ni ninii kabisa... Ningesema jambo hili, ni tendo la uumbaji la Mwenyezi Mungu; kuchukua da—damu mwilini ambayo imeharibiwa na kansa, mpaka jamaa huyo mdogo, aliyegeuka manjano na kuvimba-vimba, na katika muda wa dakika chache tu, damu mpya kabisa mwilini!

²⁴ Ninaamini...Sitanena katika Jina Lake; nitalinena katika ninii yangu...katika ufunuo wa imani yangu, yaliyotukia kule kwenye Magenge Marefu ya Sabino juzijuzi. Ninaamini ya kwamba saa yaja, wakati viungo vya mwilini vinavyokuwemo vitarudishwa, na Nguvu zenye utukufu za Muumba. Ni—ninaamini, kama Yeye anaweza kuumba kindi awepo, ambaye hana...Huyu hapa mwanamume ama mwanamke, ambaye alikuwa hana kiungo kimoja. Na huyo ni mnyama mzima, yeye mwenyewe. Yeye ni Mungu. Ni—ninampenda.

²⁵ Vema, sasa, nikiyaanza masomo hayo, ndio tutaendelea tu kuzungumza. Na huku watu wamezunguka kuta, nao wamesimama kwenye kumbi, na kwenye vyumba, na kadhalika, kwa hiyo nitaingia moja kwa moja kwenye Ujumbe huu.

²⁶ Nami ninataka kusema jambo hili, nami ninataka kumshukuru Yeye Ambaye yuko kila mahali. Na, ya kwamba, leo, bila kujua jambo moja kuhusu huo Muhuri wa Tano, Huo ulikuja katika njia ile ile ya kisiri, asubuhi ya leo, yapata tu lisaa limoja kabla ya mapambazuko, nilipokuwa kule kwenye maambi. Na leo... .

²⁷ Nimeketi tu hizi siku tano ama sita zilizopita, kwenye chumba kidogo tu, sionani na mtu ye yote. Ninatoka tu na

kwenda kula milo yangu pamoja—pamoja na rafiki mmoja, pamoja na baadhi ya marafiki zangu hapa. Na, bila shaka, mnamjua rafiki huyo ni nani, ni Ndugu na Dada Wood. Naam. Na—nanyi mwajua, nami nilienda kule na—na kukaa nao, na kila mtu amekuwa mwenye furaha. Na hapajakuwapo na cho chote, ni ninii tu. . .

²⁸ Ninajaribu kudumu moja kwa moja na huo Ujumbe wa Mihuri hii. Ni jambo muhimu. Ninaamini ni—ni—saa ya kufunuliwa Kwake, ya kufunuliwa Kwake.

²⁹ Na sasa ninawatakeni mwe na hakika sasa, mapema, kabla, mara mwezapo, andikeni mambo yenu msiyoyaelewa kuhusu—kuhusu Mihuri hii Saba, kama mnayo, na myaweke mezani. Na penginepo Ndugu Neville ama mtu fulani huenda akaweka sanduku hapa. [Mtu fulani anasema, “Hili hapa sanduku.”—Mh.] Loo! hapa—hapa, ninayaona sasa. Hilo ni jambo zuri. Afadhali niyapate usiku wa leo, ili kwamba labda nipate kuyasoma kidogo, kwa ajili ya Jumapili asubuhi. Sasa, msinini, wakati huu, wakati uu huu, msilete maombi ya, tuseme, “Je! ushuhuda wa mtu kumpokea Roho Mtakatifu ni *huu*?” Mnaona? Ni—ningetaka kujua habari ya mambo, niliyofundisha, unaona, ili tuweze kupata somo hili moja (kama vile zile nyakati za kanisa) sawasawa, unaona, kwa sababu hilo ndilo tunaloshughulikia sasa.

³⁰ Sasa, kama vile ambavyo tungelikuwa tunataka kuwaombea wagonjwa, basi hilo linataka labda ma—maombi tofauti. Nawe umetiwa upako, umekuja kwa ajili ya jambo lingine, unajua. Nawe unamsihi Mungu, kupata kujua, “Je! kutakuwa na mtu fulani kule usiku wa leo, Bwana?”

³¹ “Ndio, itakuwa ni mtu fulani aliyevaa gauni la manjano, akiketi kwenye pembe ya mkono wa kulia. Na utakapomwita mwanamke hiyo, umwite *hivi*. Na useme alifanya *kadha* na *kadha*. Na ana *kadha*.” Ndipo unashuka na kuenda kule na kuangalia, na ndiye huyo hapo. Unaona? Haya basi, unaona. Ni tofauti. Unaona?

³² Na kwa njia hii, ninaomba, “Bwana Yesu, tafsiri ya Hili ni nini? Nifunulie.” Amina.

³³ Sasa hebu na tuchomoe Mapanga ye—yetu tena sasa, na, Neno.

³⁴ Nami ninafurahia kuniunga kwake mkono kiroho Ndugu Neville, pamoja na upendano wake wa ndugu, hapa nyuma yangu, akiniombea. Na ninyi nyote huko mliko, pia. Na, sasa, usiku huu huu ukiwa ni usiku wa Ijumaa, tutajaribu, kuifanya tu kama. . . sisi. . .

³⁵ Huwezi kabisa kugusia mambo yote. U-. . .Maana, ungeweza kuchukua jambo Hilo, mmoja tu ya Mihuri hiyo, na ukae, kuihubiri tu—tu moja kwa moja kwenye Maandiko, uifuatilie kabisa. Unaona? Ingechukua miezi na miezi na

miezi, na bado hungeipata, maana Mu—Muhuri Wenyewe unafungamanisha Maandiko yote, kutoka Mwanzo mpaka Ufunuo, Muhuri mmoja wa Hayo.

³⁶ Kwa hiyo jambo ninalojaribu kufanya, ni, kujizuia nisiende mbali sana Nao, nitaandika Andiko fulani, ama—ama muhtasari mfupi mahali fulani hapa, na kujizuia nisininii... Kudumu tu kwenye jambo hilo moja, sina budi kuangalia nyuma, maana, mimi ninaninii tu...Kunena, mimi hunena kwa—kwa njia...Na—natumaini ni upako sahihi. Na halafu ninapo—ninapoangalia chini kuona ninii...Nami ni—ninaanza kuzungumza, na ninajisikia nikitoka kwenye somo fulani, nitageuka, niangalie upande mwingine, kujaribu kuchukua Andiko lingine, ili kuingilia hilo, unaona, kulirahisisha kwa namna fulani upande ule, badala ya kujaribu kuendelea na jambo hilo.

³⁷ Na kwa hiyo sasa tutasoma usiku wa leo, kwa neema ya Mungu, kwa msaada Wake, ule—ule Muhuri wa Tano. Nao ni mfupi. Ni mrefu kidogo kuliko ule mwingine. Wale wapanda farasi wanne, sasa, walikuwa aya mbili kila mmoja, na hivi ni vifungu vitatu katika huu. Sasa, Muhuri wa Tano unaanza, sura ya 6 ya Ufunuo, aya ya 9.

³⁸ Na, sasa, kama ikitokea kwamba wewe ni—ni mgeni ambaye hujawasikia hawa wapanda farasi wanne, vema, wewe... Unaona, wakati mwingine u—unarudi tu nyuma na— na kwa namna fulani unagusia jambo fulani, na, ukifanya hivyo, unawatarajia watu wafahamu jambo Hilo. Kwa hiyo kama kuna jambo fulani dogo usilofahamu, vema, hebu kwa namna fulani vumilia tu kidogo. Ama, chukua kanda na uisikilize, na—na nina hakika uta—utapata baraka Kwake. Mimi nimepata baraka. Ni—ninatumaini ya kwamba u—unaipata.

³⁹ Sasa, kila mtu tayari, kutoka aya ya 9 sasa hadi ya 11, ama pamoja na ya 11.

Na alipoifungua muhuri ya tano nikaona chini ya madhabahu roho zao waliochinjwa kwa ajili ya neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao.

Wakalia kwa sauti kuu, wakisema, Ee Mola, Mtakatifu, na Mwenye kweli, hata lini kutokuhukumu, wala kuipatia haki damu yetu kwa hao wakaao juu ya nchi?

Nao wakaopewa kila mmoja nguo ndefu, nyeupe, wakaambiwa wastarehe bado mu—muda mchache, hata itakapotimia hesabu ya wajoli wao pia...ndugu zao, watakaouawa vile vile kama wao.

⁴⁰ Sasa, kwa namna fulani jambo hili ni la kisiri. Na sasa kwa ajili ya kanda, na makasisi na waalimu wanaoketi hapa, sasa, kama una maoni tofauti na Haya; nilikuwa nayo, mimi

pia. Lakini ninayachukua tu kutokana na uvuvio, ambao ulibadilisha kabisa maoni yangu juu ya jambo Hilo. Unaona?

41 Na ndipo ninaona, kama mtakavyoona hii ikifunuliwa, Hilo linarudi moja kwa moja huko nyuma na kuunganisha hizo nyakati za kanisa na Maandiko moja kwa moja pamoja, na kulifungamanisha. Unaona? Na hiyo ndiyo sababu kwamba ninaamini ya kwamba Hilo linatoka kwa Mungu. Sasa, tunatambua jambo hilo.

42 Nami ninafikiri ya kwamba wakati mwingine kwamba tunategemea yale labda mwaalimu fulani mashuhuri alivyosema kuhusu jambo Hilo. Unaona? Na hilo—hilo ni sawa. Mimi simshutumumu mwalimu huyo, hata kidogo. Wala simshutumumu mtu ye yote. Mimi ninakemea dhambi tu, kutokuamini; sikemei mtu.

43 Na watu wengine wamesema, “Unayakaripia madhehebu.” La, siyakemei. Ni—ninalaumu utaratibu wa madhehebu; si watu waliomo humo ndani; kundi lile la watu linalofanya madhehebu hayo, mnajua. Lakini ni utaratibu ule unaowatawala, huo ndio ninaokaripia, Mkatoliki na Mprotestanti, ni mamoja. Jamani! Mimi nimeninii . . .

44 Baadhi ya marafiki wazuri sana ambao—ambao—ambao ninawajua, ni Wakatoliki, ninii tu . . .? . . . Je! mna habari . . . Na mtu huyo huenda ameketi hapa usiku wa leo, labda yuko. Njia pekee tuliyoweza kuijenga maskani hii, ni kwa sababu Mromani Katoliki mmoja alisimama kwa miguu yake kule mahakamani, na akanitetea, na, jamani, jinsi ambavyo hapana mtu ye yote angalifanya hivyo. Hiyo ni kweli. Nao wasingekataa. Hiyo ni kweli.

Naye akasema, “Walikosea katika hesabu, ‘Watu wengi kupita kiasi.’”

45 Akasema, “Loo! hilo halitakuwa na zaidi ya watu themanini kwenye kanisa lile, namna hiyo.” Kasema, “Kanisa hilo limesimama pale.” Kasema, “Mimi—mimi namjua mchungaji wake, na yote namna hiyo.” Kisha kasema, “Kanisa lile limekuwa mahali pale.” Kasema, “Wengine wenu mnaweza kuyapanua yenu, basi mbona wao wasilipanue?” Mromani Katoliki, rafiki wangu msiri. Unaona? Naam, bwana.

46 M—mvulana ambaye ni M—Mkatoliki, rafiki yangu mwaminifu kweli, alikuwa akizungumza nami. Alikuwa na duka moja la kuuza maunzi; kabla sijaondoka. Akasema, “Billy, ni—ninajua wewe hukubaliani na utararibu wetu wa dini.” Akasema, “Lakini ninakwambia sasa hivi,” akasema, “Mungu ameheshimu maombi yako sana kwa ajili yetu! Ninaamini, kama ukipata shida mahali po pote nchini,” kasema, “kila Mkatoliki nchini angekuja kukusaidia.” Kwa hiyo, unaona, hilo ni . . .

47 Akasema, “Kila msalaba—mgongoni,” ndivyo alivyowaita. Nitalisema jinsi tu alivyolisema. Bila shaka, wao wanadai kuwa hivyo ati kwa sababu Wakristo wa mwanzoni walibeba misalaba

migongoni mwao. Tunajua jambo hilo kwa historia. Nao wanadai kwamba wao ndio yule Mkristo wa mwanzoni, ambao ndivyo walivyokuwa, lakini madhehebu yao yamewaondoa kwenye ile njia, mnaona.

⁴⁸ Na hao watu, Mkatoliki, ama Myahudi, ama ye yote yule awaye, wao ni wanadamu kutoka kwenye mti ule ule tuliitoka. Mnaona? Hiyo ni kweli. Wao—wao ni watu ambao wanapenda, na wanakula, na kunywa, na kulala, na kama tu mtu mwingine ye yote. Na kwa hiyo haitupasi kamwe kuwashutumu watu binafsi, la, hata mmoja, unaona. Lakini, haitupasi kuwachukia watu binafsi.

⁴⁹ Lakini, kama mhudumu, sina budi kumpiga yule nyoka mahali pale alipo, ambaye anawauma watu hao, mnaona. Na mimi si—hata si—. . . Mimi peke, na mimi mwenyewe, nisingefanya jambo hilo kama halingekuwa ni agizo kutoka kwa Mungu, ya kwamba ninawajibika kufanya jambo hilo, unaona. Nami sina budi kushikilia hilo kwa ukweli na uaminifu.

⁵⁰ Lakini kama Mkatoliki, Myahudi, ama ye yote yule angekuwa, akija hapa; kama yeye angelikuwa ni Mwislamu, Myunani, ama Muorthodoksi, ama angekuwa cho chote kile. Kama akija hapa kuombewa, ningeomba kwa uaminifu tu kwa ajili yake kama vile ningaliomba kwa ajili ya walio wangu. Hiyo ni kweli. Hakika, kwa maana yeye ni binadamu. Nami nimewaombea Wabudha, na Makalasinga, Wajaini, Waislamu, na—na wa kila aina, unaona, namna hiyo. Na siwaulizi maswali yo yote; ninawaombea tu, kwa sababu wao ni mtu fulani, mwanadamu anayetaka kupona, na kujaribu kuyafanya maisha kuwa rahisi kidogo njiani kwa ajili yao.

⁵¹ Sasa tunatambua, ya kwamba, katika jambo hili, na wengine wenu hapa ninajua, kuna wanachuoni halisi kama wawili ama watatu wanaoketi hapa. Na—nao ni werevu, nao wamesoma ma—mafundisho ya watu wengine juu ya somo hili. Nami ninawataka ndugu hawa wajue ya kwamba mimi si—siwalaumu watu hawa. Mimi ninatamka tu yale Bwana anayonionyesha. Na hayo tu ndiyo niliyo nayo.

⁵² Sasa, hatutaki kamwe kuwazia jambo hilo, kwa sababu maskini mwanamke fulani dobi ama—ama maskini mvulana mkulima mmoja kule nje, hangeweza kupata ufunuo kutoka kwa Mungu. Kwa sababu, unaona, ni . . . Mungu, Yeye kweli hujifunua Mwenyewe katika urahisi. Hilo ni, tulikuwa nalo Jumapili ile, kuanzia jambo hili, jinsi Yeye anavyojifunua katika urahisi Wake. Hilo ndilo linalomfanya Yeye kuwa Mkuu.

⁵³ Sasa hebu—hebu ni ninii tu. . . Hebu nirudie tu hayo kwa muda kidogo tu. Kile kinachomfanya Mungu kuwa mkuu, ni kwa sababu Yeye anaweza kujifanya rahisi sana. Hicho ndicho kinachomfanya Yeye kuwa mkuu. Mungu ni mkuu, Naye anaweza kujiweka Mwenyewe katika namna rahisi sana mpaka

walio na hekima ya ulimwengu huu hawawezi kumpata Yeye. Wao hawawezi tu kumpata Yeye, kwa maana Yeye hujifanya rahisi mno. Sasa angalia. Na jambo hili, lenyewe, ni siri ya ufunuo wa Yesu Kristo. Unaona? Hili, lenyewe, ambalo ninii. . . Kuna. . . hakuwezi kuwako na kitu kilicho kikuu kuliko Mungu. Wala huwezi kufanya cho chote kiwe rahisi kama Yeye anavyojifanya rahisi. Unaona, hicho ndicho kinachomfanya kuwa mkuu. Unaona?

⁵⁴ Sasa, mtu aliye mkuu, anaweza tu kuwa mkuu zaidi kidogo, ama labda anaweza kujidhili na kukuambia, “U hali gani?” wewe, unaona ama kitu kama hicho. Lakini hawezi kujishusha. Kuna kitu fulani tu alichu. Yeye ni mwanadamu. Yeye hawezi tu kujishusha. Maana, wakati anapojishusha kupita kiasi, basi, muda si muda wajua, hana budi kuzungumzia yale mtu mwingine aliyofanya, na kitu kama hicho. Na halafu anaanza kujivuta juu tena, unaona.

Lakini, njia ya kupanda ni kushuka, katika Mungu. Naam.

⁵⁵ Wenye elimu wa ulimwengu wanajaribu, katika maarifa yao, kumpata Yeye. Wao wanapanda tu juu mbali na Yeye, wakifanya hivyo. Unaona, wenye maarifa wa dunia hii, kama unajaribu kuelezea jambo fulani kwa hisabati fulani ama cho chote kile. Kumbuka, Yeye hata ameliweka. . . Katika Biblia, katika Ufu- . . . La, samahani.

⁵⁶ Isaya 35, ninaamini ndiyo, ya kwamba hata ni ra—rahisi sana hata mtu m—mjinga angelilifahamu, unaona. Vema, “Ajapokuwa mjinga hatapotea katika njia hiyo.”

⁵⁷ Wenye maarifa hulikosa kwa mbali, kwa maarifa yao, wakienda mbali Naye, kwa kujaribu kumpata Yeye kwa maarifa. Sasa, msisahau hilo. Hilo litarekodiwa kwenye kanda, unaona. Wenye maarifa, katika maarifa yao, wanaenda mbali sana wakijaribu kumtafuta kwa maarifa yao, wanamkosa, unaona. Laiti wao wangalikuwa wakubwa vya kutosha kuwa rahisi vya kutosha, wangeweza kumpata. Kama wewe u mkubwa vya kutosha kuwa rahisi vya kutosha! Unaona hilo? Na, unanajua, hilo—hilo kwa kweli ni Kweli.

⁵⁸ Nimeenda kwa watu, kwenye afisi zao, na kadhalika, waliokuwa kweli ni wanaume kweli, wakubwa, wafalme, unaona, na watawala, masultani, na kwa kawaida hao ni watu wakubwa. Halafu, nimeenda mahali ambapo jamaa fulani ana nguo za kubadilisha, labda mhudumu fulani aliyetaka kubishana nami kidogo, na unge—ungefikiri ya kwamba ulimwengu haungeweza kuendelea bila ya yeye, unaona. Na huko—huko ni kujaa majivuno tu kichwani, unaona. Lakini, m—mtu mkubwa, mtu mkubwa huketi chini na kujaribu kukufanya ufikiri wewe ndiwe mtu mkubwa. Unaona? Unaona, yeye anaweza kujinyenyekeza.

59 Na, unaona, Mungu ni mkuu sana hata anaweza kujinyenyekeza, kufikia mahali, ambapo mwanadamu hawezi kujishusha umbali huo, unaona. Basi. Na katika ninii zao. . .

60 Nao wanajaribu kumtafuta. Sasa angalia. Wanajaribu kumpata kwa kuwapeleka vijana shuleni, na kupata Shahada ya Sanaa. Na—na wanajaribu kumpata kwa istilahi ya kitheolojia ya—ya—ya—ya Biblia. Na wanajaribu kumpata kwa miradi ya elimu, na kwa taratibu za kimadhehebu, na kwa kupambapamba mambo, na kujaribu kutafuta. Yeye hayuko huko, hata kidogo. Unafanya tu kazi bure, ni hivyo tu. Una—unaenda tu mbali na jambo Lenyewe

61 Wangeweza kuwa wakubwa vya kutosha kuwa—kuwa wanyofu vya kutosha, wangeweza kumpata Yeye katika mwelekeo huo, kwa wao kuwa wanyofu. Lakini mradi tu unaelekea kwenye elimu, unaenda mbali na Yeye.

62 Sasa hebu nichukue hilo kusudi msilikose. Mradi tu unajaribu kumpata Mungu kwa maarifa, kama ilivyokuwa katika bustani ya Edeni, kama ilivyokuwa katika siku za Musa, kama ilivyokuwa katika siku za—za Nuhu, kama ilivyokuwa katika siku za Kristo, katika siku za Yohana, katika siku za mitume, na hadi siku hii! Unapojaribu kumwazia, na kujaribu kumpata Mungu kwa maarifa, daima unaenda mbali naye. Unajitahidi kumwelewa Yeye. Hakuna njia ya kufanya jambo hilo. Likubali tu. Unaona? Liamini tu. Usijaribu kulielewa.

63 Siwezi kufahamu kwa nini, kwamba, vema, mambo mengi sana. Si mambo mengi ninayoelewa ama ninayoweza kuyaelewa. Siwezi kuelewa jinsi ambavyo kijana huyu mdogo anayeketi hapa anakula chakula kile kile ninachoweza kula, na—na, yeye hapa, kichwa kimejaa nywele, mimi sina zo zote. Sielewi hilo. Wananiambia ya kwamba kasiamu huitengeneza; na siwezi kuweka kucha zangu ya vidole vya mikono zikae muda mrefu vya kutosha bila kuzikata, na huku sina nywele zo zote za kukata. Si—sielewi na hilo. Kama ulivyo ule msemu wa kale, mimi. . .

64 Si kwamba ninabadilisha msimamo kwa namna fulani, ule uzito; lakini, Huo ni uzito, lakini ningali bado sijaufikia ule Muhuri.

65 Jinsi ambavyo ng'ombe mweusi anavyoweza kula nyasi za kijani kibichi, na kutoa maziwa meupe, ambayo yakisukwa-sukwa hutoa siagi ya manjano! Hakika si—singeweza kuelezea jambo hilo, unaona. Maana, unaona, kila kimoja hutokana na kingine. Na jinsi jambo hilo linavyotendeka, mimi siwezi kuelezea.

66 Siwezi kueleza jinsi mayungi mawili yanavyosimama, ama maua mawili, ya aina moja, na moja ni jekundu, na hilo lingine la kimanjano, na moja la hudhurungi, na moja la samawati. Sifahamu hilo. Jua lile lile linalowaka juu yao. Hiyoy rangi

inatoka wapi? Unaona? Si-siwezi kueleza jambo hilo, lakini hata hivyo huna budi kulikubali.

⁶⁷ Laiti tu mwanatheolojia mmoja mashuhuri angalinieleza jinsi dunia hii inavyozunguka katika obiti. Laiti ungaliweza kunitupia mpira hewani, unaovingirika, na uufanye ufanye mzunguko wa pili, mahali pale pale. Hungeweza kufanya hivyo. Na hata hivyo huu umepimwa kikamilifu sana hata wao wanaweza kujua kupatwa kwa jua kwa usahihi wa dakika moja, miaka ishirini tangu sasa. Hawana saa ya mkono ama ya mezani, ama namna yo yote ya mtambo, ambao ni mkamilifu namna hiyo. Na hata hivyo dunia inasimama pale. Na, halafu, imelala kwa nyuma. Vipi kama ingalinyoka kidogo? Naam. Unajifanya tu mjinga, kujaribu, unaona.

⁶⁸ Kwa hiyo, unaona, usijaribu kupata maarifa, kuelewa. Amini tu yale asemayo Yeye. Na jinsi unavyoweza kuwa mnyofu zaidi, hivyo ndivyo inavyotakiwa, utampata. Sasa, ninashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo, ninashukuru sana jinsi alivyo Yeye, amejishusha Mwenyewe. Sasa, tunaona, sura ya 6 na aya ya 9. Hebu nianze sasa.

Na alipoifungua muhuri ya tano, nikaona chini ya madhabahu roho zao waliochijwa kwa ajili ya neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao.

⁶⁹ Angalia, hakuna kutajwa kwa Mnyama mwingine, ama Mwenye uhai—Mwenye uhai, kwenye huku kutangazwa kwa Muhuri wa Tano. Sasa kumbuka, alikuwako, kwenye Muhuri wa Nne. Alikuwako, kwenye Muhuri wa Kwanza, wa Pili, wa Tatu, na wa Nne, lakini hakuna ye yote hapa. Unaona?

⁷⁰ Sasa, kama ukiangalia, hebu na tusome tu nyuma, moja ya ile Mihuri. Hebu na turudi kwenye Muhuri wa Nne, unaona. Na hiyo ni aya ya 7.

Na alipoifungua muhuri ya nne, nikasikia sauti ya yule mwenye uhai wa nne akisema, Njoo uone!

. . . alipoi- . . . alipoifungua muhuri ya tatu, nikasikia sauti ya—ya yule mwenye uhai wa tatu akisema, Njoo uone!

. . . ya mwenye uhai wa pili, . . . Njoo uone!

. . . na mwenye uhai wa kwanza, Njoo uone!

⁷¹ Lakini tunapofikia Muhuri wa Tano, hakuna Mnyama. Sasa angalia tu.

Na alipoifungua muhuri ya tano, nikaona chini ya madhabahu . . .

⁷² Upesi sana! Unaona, hakuna—hakuna Mwenye Uhai pale. Na Mnyama anawakilisha nguvu. Tunajua jambo hilo, unaona. Hakuna Mwenye Uhai.

⁷³ Sasa, mmoja wa hao Wenye Uhai, tunaona, katika kusoma ule—ule—ule ufunuo katika makanisa, ya kwamba mmoja wao alikuwa . . . alikuwa ni simba; na huyo mwingine—huyo mwingine alikuwa ni ndama; na huyo mwingine alikuwa ni mwanadamu; na huyo mwingine alikuwa ni tai. Tunaona, katika nyakati za kanisa, ya kwamba hao Wenye Uhai wanne, wakimaanisha nguvu nne, walikuwa wamekizunguka Matendo ya Mitume, jinsi tu vile ile—ile maskani jangwani. Nanyi mnafahamu jambo hilo, maana sitachukua wakati kuingilia jambo hilo. Jinsi tulivyolichora hapa, na kuonyesha vile ilivyokuwa hasa! Wao walikuwa wakilinda Hili, Mwana-Kondoo na Neno, kulitimiza Neno kama tu walivyofanya na lile—lile sanduku la agano katika Mahali Patakatifu kule jangwani, na kadhalika.

⁷⁴ Sasa, hata tulionyesha jinsi walivyokaa, kwa bendera za kabila za Israeli, na kwa . . . Ni wangapi waliosikia zile saba—zile nyakati saba za kanisa? Nadhani karibu wote mmesikia, theluthi mbili yenu. Angalia, ya kwamba hata ile tabia ya yule Mwenye Uhai ilikuwa ni nembo kabisa ya kabila, jinsi wale wanne . . . yale makabila kumi na mawili yalivyokaa, manne kila upande, ama—ama makabila matatu kila upande. Na wale Wanyama wanne waliketi na kuangalia, makabila haya, kutoka njia zote nne.

⁷⁵ Na, wakati, tulipokwenda na tukachukua zile Injili, na kuonyesha vizuri kabisa. Unapokwenda kwenye lile sanduku, wao walikuwa wakililinda sanduku, lile agano. Na halafu tunaona ya kwamba lile agano la Kanisa jipya, kuwakilishwa Kwake duniani, kulikuwa ni Roho Mtakatifu. Ile damu ilikuwa imeturudishia, sisi, Roho Mtakatifu. Na wale Wenye Uhai wanne waliwakilisha, na kama vile yale makabila kumi na mawili ya Israeli, walipokuwa wanaangalia. Na tunaona tabia zao walivyo, na kuchukua tabia hiyo hiyo na kuileta kwenye kila moja ya hizo Injili nne, hasa, walikuwa ni jambo lile lile. Mmoja alizungumza na simba, yule mwingine na ndama, na huyo mwingine . . . Zile Injili nne! Hizo hapo. Zile Injili nne ni ulinzi wa Roho Mtakatifu. Amina.

⁷⁶ Daima mimi hushangaa tu . . . Limedumu moyoni mwangu. Sasa, hii ni kama miaka sita, nadhani, tangu nimsikie mtu mmoja mashuhuri akisema ya kwamba hicho kilikuwa ninii . . . “Matendo ya Mitume kilikuwa tu ni fremu ya jengo.” Nimesikia jambo hilo likisemwa mara nyingi. Lakini kumsikia mtu mwenye wadhifa aliokuwa nao, kama mhubiri na kama mwalimu, ambaye ameandika baadhi ya vitabu vinavyojulikana sana ambavyo watu wanavisoma kila mahali, na kusema ya kwamba Matendo ya Mitume hakikufaa kweli kwa mafundisho ya Kanisa!

⁷⁷ Ambapo, Matendo ya Mitume ndicho msingi Wake hasa; si fremu. Ati msingi! Maana, Biblia inasema ya kwamba m—m—

m—msingi wa Mungu “umejengwa juu ya Fundisho la mitume,” kweli, “Kristo, Kichwa, Jiwe la pembeni.”

⁷⁸ Na wakati jamaa huyu aliposimama pale na kutoa tamshi hilo, mimi—mimi—mimi—nilininii tu. . . Moyo wangu ulizimia tu. Ndipo nikawaza, “Si ajabu.” Vema, sasa ninaona, katika ile Mihuri. Ni kwamba tu halikuwa limefunuliwa. Ni hivyo tu. Unaona?

⁷⁹ Kwa hiyo, kuhusu hilo, walikuwa ndio hao hapo, wamesimama pale, lakini kulikuwa na kitu fulani kilichokuwa kikisema tu jambo hilo. Sasa, angalieni, wanalinda.

⁸⁰ Sasa, wakati tulipochukua Mathayo 28:19, na kufuatilia jambo hilo katika Mathayo, ambaye alimwakilisha yule simba. Na tukija, humo ndani, tuliona ni kwa nini hasa wao wanabatiza katika Jina la Yesu Kristo. Huyu hapo, akisimama pale na Andiko lilo hilo, kulinda lile agizo takatifu la ubatizo, wa Jina la Yesu Kristo. Vema. Vema, ninaenda kando kwa kuingilia nyakati za kanisa sasa.

⁸¹ Angalia. Lakini, hapa, tunapokuja kwenye Muhuri huu wa Tano sasa, hakuna—hakuna—hakuna mpanda farasi anayetoka kwenda, wala hakuna Mwenye Uhai wa kuutangaza. Yohana alininii tu. . . Mwana-Kondoo aliufungua, na Yohana akauona. Hapakuwapo na mtu hapo wa kusema, “Sasa njoo, utazame. Njoo, uone.” Angalia, hapakuwapo na nguvu za huyo Mwenye Uhai. Ama hakuna. . .

⁸² Na kwenye ule Muhuri wa Sita, hakuna Mwenye Uhai wa kuutangaza. Na kwenye Muhuri wa Saba, hakuna Mwenye Uhai wa kuutangaza. Hakuna nguvu za kuutangaza. Unaona, hakuna mtu anayeutangaza. Kwenye ninii. . . Angalia. Kwenye ninii. . . Baada ya Muhuri wa Nne, hakuna tangazo la nguvu zo zote za Mwenye Uhai, kutoka Muhuri wa Tano, Sita, ama wa Saba, hakuna kabisa.

⁸³ Sasa angalia. Ninapenda jambo hili. Kama vile katika wakati wa yule mpanda farasi wa wale farasi wanne, yule mpanda farasi (umoja) wa wale farasi wa nne tofauti, kulikuwako na Mnyama ambaye alitangaza zile nguvu. Kila wakati huyo mpanda farasi alipomtandika farasi mwingine na akaja kumpanda, Mwenye Uhai wa aina nyingine alitokea na kutangaza jambo hilo, “Hiyo ni siri kuu.” Unaona? “Hiyo ndiyo ile siri.” Kwa nini? Anatangaza siri.

⁸⁴ Kwa nini hakuna mtu hapa kwenye Muhuri wa Tano, kuutangaza? Ni hivi, kulingana na ufunuo ambao Bwana Yesu alinipa leo, unaona, ama asubuhi ya leo, alfajiri. Hiyo ni, kwa sababu, ile siri ya nyakati za kanisa imekwisha tayari, kwenye wakati huu. Ile siri ya mpinga-Kristo imefunuliwa, kwenye wakati huu. Mpinga-Kristo aliendesha farasi mara yake ya mwisho, nasi tulimwona kwenye farasi wake wa kijivujivu,

amechanganyika katika rangi zake nyingi, naye anaenda moja kwa moja mpaka upotevuini.

⁸⁵ Tutapata jambo hilo kwenye zile Baragumu, na kadhalika, tutakapofundisha jambo hilo. Ningeliliendea sasa, lakini tutaondoka kabisa kwenye somo hili tena. Nasi—nasi tunaenda...yeye anaenda...

⁸⁶ Hiyo ndiyo sababu hakuna mtu pale. Sasa, sisi hatuna sababu iliyoandikwa, sababu fulani ya jambo fulani. Basi, mnakumbuka, mara ya kwanza, mwanzoni, nilisema hapawezi kuwapo na kitu kisicho na sababu yake. Mnakumbuka lile tone dogo la wino? Mnaona? Lakini huna budi kupata sababu yake. Kuna sababu fulani ya wao kutokuwa na Mwenye Uhai, ama nguvu, kutangaza Muhuri huu unapovunjwa. Na Mungu tu Ndiye anayeweza kufunua sababu yake, hivyo tu, kwa sababu yote—yote ni juu Yake.

⁸⁷ Lakini sababu ya Yeye kuufunua, ninavyofahamu mimi, ni kwamba ile siri ya Kitabu cha Ukombozi, kuhusu mpinga-Kristo kufunuliwa; na katika wakati ule ule, Kanisa limeondoka, na mambo haya hata hayatendeki katika wakati wa kanisa, hata kidogo. Hiyo ni kweli. Hayo yako—yako mbali na wakati wa kanisa. Kanisa limenyakuliwa kabisa, wakati huu. Kanisa linapaa juu, katika sura ya 4 ya Ufunuo, na halirudi mpaka linaporudi pamoja na Mfalme Wake, katika sura ya 19. Lakini Mihuri hii hapa inafunua yale yaliyoko, yale yaliyoko, na yale yatakayokuja. Unaona? Na, sasa, kile wakati wa kanisa ulipaswa kuwa, kilifunuliwa na Mihuri hii. Na sasa angalia yale yanayotokea.

⁸⁸ Zile—zile hatua nne za mpanda farasi wake zimefunuliwa. Zile hatua nne za mpinga-Kristo, akipanda farasi, zimefunuliwa wakati huu, kwa hiyo haiwalazimu kuwapo tena.

⁸⁹ Na kulikuwako na wale Wenye Uhai wanne wa Mungu, kumtangaza yule mpanda farasi alipokuwa amempanda farasi. Wenye Uhai wanne ni nguvu nne. Sasa, tunajua ya kwamba *Mnyama*, kwa tafsiri ya maneno ya mifano ya Biblia, maana yake ni “nguvu.” Sasa, hebu na tuelewe na jambo hilo vizuri. Hao wanne ni Wenye Uhai, katika Biblia, wanawakilisha nguvu fulani miongoni mwa watu.

⁹⁰ Sasa, kama tukijua, kama vile katika Danieli, wakati alipoona taifa fulani likiinuka, ingekuwa labda ni dubu ameshikilia ubavu ubavuni mwake, katika mfano. Kisha akaona nguvu nyingine ikiinuka, mbuzi. Aliwakilisha kitu fulani. Kisha akaona nguvu nyingine ikiinuka, na—na ilikuwa ni chui mwenye vichwa vingi. Aliwakilisha ufalme fulani. Kisha akaona mwingine akiinuka, simba mkubwa sana mwenye meno, na—na aliponda-ponda yale mabaki. Huyo aliwakilisha nguvu tofauti, kabisa. Mmoja ulikuwa ni u—ufalme wa Nebukadreza; na mwingine, mfano wa—wa ndoto. Danieli aliona ono;

Nebukadreza aliota ndoto. Lakini Danieli alitafsiri ndoto yake, nayo ililingana kikamilifu na lile ono.

⁹¹ Amina! Whiu! Loo! [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.] Laiti mngalijua jambo lililotukia! Yaliyotukia kabla ya sisi kuondoka hapa? Mnaelewa? Mbona, ndoto sita mfululizo ziliambatana kabisa na lile ono. Amina. Unaona? Ndoto, ikiishafasiriwa, ni ono. Kwa sababu mtu labda hakuzaliwa na dhamira yake ya ndani akae awe amekaa macho, wakati anapooona jambo, basi Mungu huingia kwenye dhamira hii na kuzungumza naye. Ambapo, Yeye aliahidi ya kwamba, katika ndoto, katika siku za mwisho, Yeye angewazuru watu, na pia katika maono. Unaona?

⁹² Sasa, ono ni wakati uko macho kabisa, umesimama moja kwa moja namna hii, na mambo fulani yanafunuliwa. Nawe unasimama, unawaambia vizuri tu habari hiyo; unaona yaliyotukia, na yatakayotukia, na kadhalika.

⁹³ Lakini, sasa, ndoto ni wakati wewe umelala usingizi, na fahamu zako tano hazifanyi kazi, nawe—nawe uko macho kwenye dhamira yako ya ndani. Uko mahali fulani, kwa sababu, unaporudi, unakumbuka mahali ulipokuwa, unapakumbuka maishani mwako mwote. Unaona? Kwa hiyo, ni dhamira yako ya ndani. Halafu kusudi, unaona . . .

⁹⁴ Kama vile Mbunge Upshaw alivyozoea kusema, “Huwezi kuwa kitu usicho.” Na hilo ni karibu kweli, unaona.

⁹⁵ Na, basi, kama ukizaliwa mwonaji. Sasa, unaona, ili kufanya jambo hilo, hizo dhamira mbili hazina budi kukaa kabisa pamoja; si moja *hapa* ikiwa na hisi tano, zinazofanya kazi, ile nyingine *hapa* nje wakati umelala usingizi, na zile hisi tano hazifanyi kazi. Lakini, unaona, wakati zote mbili, wewe unazaliwa, zikiwa pamoja, wewe hulali usingizi. Unatoka tu kutoka moja kuingia katika ile nyingine, namna—namna hiyo. Hulali. Hakuna nafasi ya kutosha kulala usingizi. Nawe huwezi kujifanya wewe mwenyewe kuwa hivyo.

⁹⁶ Kwa hiyo, “Karama na miito vimekusudiwa na Mungu tangu zamani.” Hizo—hizo ni karama za Mungu na miito Yake, hata “havina majuto,” Biblia ilisema. Unaona? Zilikusudiwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Unaona?

⁹⁷ Sasa, sasa, tunaona ya kwamba yule . . . Mnyama, wa Danieli, ilimaanisha ya kwamba ilikuwa ni nguvu iliyokuwa ikiinuka miongoni mwa watu. Vema. Na—na maono ya Yohana hapa, pia, yalionyeshwa ya kwamba zilikuwa ni nguvu, mataifa yakiinuka. Kama vile, Marekani inavyojitokeza katika Ufunuo 13, kama mwana-kondoo. Halafu basi kama ukitaka kujua, tofauti . . .

Unasema, “Vema, hiyo, hiyo inazungumzia juu ya nguvu za kitaifa.”

⁹⁸ Anawakilisha pia nguvu takatifu, pia, mnyama. Ulijua jambo hilo?

⁹⁹ Angalia Rebeka; wakati—wakati yule—yule mtumishi wa Ibrahimu, Eliezeri... Wakati alipokuja kumchukua— beka—Rebeka, yeye... Alimpandisha juu ya ngamia, ngamia yule yule aliyemnywesha maji. Naye alimpanda ngamia huyu, apate kumlaki bwana-arusi wake asiyeonekana. Kitu kile kile alichokinywesha maji, ndicho kitu kilichompeleka kwenye makao yake ya baadaye na kwa mumewe.

¹⁰⁰ Na ni jambo lile lile leo, unaona. Kitu kile kile ambacho Kanisa linakitilia maji, hicho ni ile Mbegu, Mbegu ya Neno. Ni Neno lile lile linalokuwa hai na kutupeleka kwa Bwana Arusi wetu asiyeonekana. Unaona? Unaona?

¹⁰¹ Na angalia jinsi lilivyo kamilifu. Isaka alikuwa ameondoka nyumbani, naye alikuwa huko makondeni, mbali na nyumbani kwake, wakati Rebeka alipomwona.

¹⁰² Nalo Kanisa linamlaki Kristo hewani, na halafu Yeye anamchukua Nyumbani, Nyumbani kwa Baba, mahali ambako majumba makubwa yameandaliwa. Isaka alimchukua Rebeka vile vile.

¹⁰³ Basi, angalia, ilikuwa ni upendo walipokutana mara ya kwanza. Loo! jamani! Rebeka alikimbia tu kwenda kumlaki.

¹⁰⁴ Na hivyo ndivyo Kanisa litakavyumlaki Kristo, hewani, na liwe pamoja naye milele.

¹⁰⁵ Sasa, kwa maneno ya Biblia, Wenye Uhai hawa ni nguvu. Uone. Ninataka, sasa, ninataka mwone.

¹⁰⁶ Ibilisi alikuwa na wanyama wake wanne, wenye rangi inayobadilika, wa kupanda. Alikuwa na wanyama wake wanne. Ilikuwa ni hao wote watatu, wamewekwa katika rangi ya mmoja, na kumfanya huyo farasi mmoja kuwa wa—wa kijivujivu; farasi mweupe, farasi mwekundu, farasi mweusi. Nasi tuliona, kila mmoja wa hao ilikuwa ni hatua moja ya huduma yake, hatua ya kanisa la mwanzoni, lililokuwa limefanyika madhehebu, kule Nikea. Lile kanisa la Kipentekoste la asili, ambalo Roho Mtakatifu alimwagwa juu yake, liliposonga mbele, likachukua roho ya mpinga-Kristo, likaunda madhehebu, likazaa mabinti wa kimadhehebu. Akibadilisha nguvu zake mara tatu, na kuziweka katika mmoja, na kufanya farasi wa kijivujivu. Ndipo akapewa jina linaloitwa Mauti, naye akampanda mpaka Umilele. Ni dhahiri tu kama liwezavyo kuwa! Sasa, sasa angalia, yeye amepewa huyu—farasi huyu, naye anampanda.

Mungu, Mungu ameninii, pia, kama ilivyo kila mara . . .

¹⁰⁷ Sasa angalia. Wakati mpinga-Kristo alipotokea, kwanza, yeye alitokea katika nini? Farasi mweupe. Unaona, mbona, hana madhara kama alivyoweza kuwa, alikuwa ni fundisho tu kanisani. Wao walitaka ushirika. Ushirika wako ni pamoja

na Kristo. Lakini wao walitaka ushirika. Wao hawakuweza kuvumilia jambo hilo kamwe, walitaka kupata. . .

108 Vema, unajua, kama vile vijikundi vidogo vidogo vitakavyoinuka kanisani. Ninyi, mnajua hilo, ninyi wachungaji. Unaona? Wao, kama wanavyosema, “Kila ndege na wimbile.” Lakini kama tumezaliwa mara ya pili, ndugu, huo—huo sio msimamo wa kuchukua, unaona. La. Sasa, sisi—sisi—sisi. . .

109 Kama tukiona jambo fulani baya katika ndugu zetu, hebu na tuombe tu na kuliweka mbele za Mungu, na kumpenda mtu huyo mpaka tutakapomleta moja kwa moja katika Uwepo wa Mungu. Unaona? Hiyo ndiyo njia, njia halisi ya kufanya jambo hilo.

110 Unajua, Yesu alisema. “Kutakuwako na magugu mle ndani,” kwa maana Yesu alisema yangukwako, “lakini msiyang’oe; mtang’oa ngano pamoja nayo.” Unaona, “Waache tu.” Yeye atafanya. . . Mwache Yeye atenganishe wakati utakapowadia. Unaona? Acha yote yakue pamoja.

111 Angalia, wakati yule mnyama alipotoka, mpinga-Kristo alitoka akiwa juu ya mnyama, nguvu zake.

112 Loo! ninapenda jambo hili! Ninaanza tu kujisikia wa kiroho sasa hivi, unaona, labda lile changamko. Angalia, wakati mpinga-Kristo. . . Loo! hayo—hayo mafunuo, katika Uwepo wa ule mpira wa Moto unaoning’inia mle chumbani! Mpaka. . . Loo! ndugu! Ingawa nimeiona Hiyo, tangu nilipokuwa mtoto mchanga, kila wakati inapokuja karibu nami, inanishtua sana. Yeye karibu huniweka katika hali ya kuzirai. Huizoei Hiyo kamwe; huwezi. Ni takatifu sana.

113 Angalia, wakati mpinga-Kristo alipotoka (wanne) akaeda zake amepanda wanyama wake wa huduma, pale, Mungu alimtuma Mwenye Uhai fulani kupigana naye. Unaona? Sasa angalia. Halafu, kila wakati (yule mnyama alipopanda farasi) juu ya farasi wake, mpinga-Kristo alipompanda farasi wake, juu ya mnyama wake, kuitangaza huduma yake; Mungu alimtuma Mwenye Uhai Wake, pia, Naye alikuwa juu ya Huyo, kutangaza vita naye.

114 Sasa, Maandiko yanasema, “Adui anapoingia kama mafuriko, Roho wa Mungu huinua beramu dhidi yake.”

115 Na kwa hiyo wakati adui alipotoka akaenda zake kama mpinga-Kristo; Mungu alituma namna fulani ya nguvu kukabiliana naye. Na halafu wakati hao. . .

116 Akatoka tena, kama mpanda farasi mwekundu, rangi nyingine, nguvu nyingine, huduma nyingine; Mungu akamtuma mwingine amfuate, kupigana naye, kulishikilia Kanisa Lake.

117 Akamtuma wa tatu; tena, Mungu akatuma Wake, Mwenye Uhai wa tatu akaja na kutangaza jambo hilo.

118 Akamtuma wa nne; Mungu akamtuma Wake wa nne. Ndiyo mpinga-Kristo akaisha, na nyakati za kanisa zikaisha, pia, wakati huo. Angalia. Sasa loo! hili ni zuri kwelikweli!

119 Sasa, tunaona ya kwamba ibilisi anabadilika, wanyama—wanyama wanne, walimaanisha walifunuliwa kuwa nguvu gani kwa... ama ni nguvu gani aliyoufunulia ulimwengu, na jinsi wao walivyoishia katika farasi huyu wa kijivujivu, wa “mauti.”

120 Sasa na hebu na tuangalie nguvu za Mungu, za Wenye Uhai hawa, za kupigana nao.

121 Mwenye Uhai wa Kwanza wa Mungu, aliyekwenda naye kumkabili mpinga-Kristo, ile roho ya mpinga-Kristo wakati ilipokuwa katika kufundisha kwake tu. Sasa kumbukeni, wakati mpinga-Kristo alipopanda farasi mara ya kwanza, yeye alikuwa katika huduma ya kufundisha. Mpinga-Kristo alipanda farasi, mara ya kwanza, katika huduma ya kufundisha. Sasa angalia yule aliyeenda kumkabili: simba, Simba wa kabila ya Yuda, ambaye ni Neno. Wakati fundisho lake la uongo lilipotoka, Neno la kweli lilikwenda kukabiliana naye.

122 Hiyo ndiyo sababu tulikuwa na akina Ireneo, na Polikapu, na—na—na—na jamaa hao, akina Mtakatifu Martin.

123 Wakati huyo mpinga-Kristo alipokuwa anapanda farasi na mafundisho yake ya uongo; Mungu alituma Fundisho Lake, Neno, Simba wa kabila la Yuda, ambaye ni Neno lililodhihirishwa katika Roho Mtakatifu. Na Roho Mtakatifu, pale, kujidhihirisha Mwenyewe, ambaye ni Neno!

124 Hiyo ndiyo sababu Kanisa la mwanzoni lilikuwa na uponyaji, na miujiza, na maono, na nguvu, ni kwa sababu ilikuwa ni Neno lililo hai, katika mfano wa Simba wa kabila la Yuda, akipanda farasi kwenda kukabiliana na huyo. Amina! Sasa mmelipata? Yeye hutuma nguvu zake, mpinga-Kristo; Mungu anatuma Zake, Neno. Mpinga-Kristo, fundisho la uongo; Fundisho la kweli lilifuatana nalo, kupinga fundisho hilo! Sasa, huyo alikuwa ni yule wa kwanza. Sasa, hili lilikuwa ni Kanisa la kwanza, la kimitume, lililotoka kwenda kukabiliana naye.

125 Sasa, mnyama wa pili ambaye mpinga-Kristo alimtuma, alikuwa ni farasi mwekundu, ambaye alikuwa aninii... ambaye alimpanda, alikuwa aondoe amani (na) duniani, na—na afanye vita.

126 Sasa, wa pili aliyeondoka kwenda kukabiliana naye, alikuwa ni Mnyama ndama. Ndama maana yake ni kazi, Mnyama wa kazi.

127 Na sasa kama tungeweza tu kusimama kwa dakika moja. Hebu ni ninii, naam, hebu ni ninii, ili kwamba tu mwe na hakika ya kuona jambo hili sasa. Sasa, hilo ni la namna ambayo huenda kidogo ikawatatiza. Lakini hebu na tuchukue Thiatira hapa. Angalia uone kama si Ka—Ka—Kanisa chapa kazi, mnaona.

*Na kwa malaika wa kanisa lililoko Thiatira andika;
Haya ndiyo anenayo Mwana wa Mungu, yeye aliye na
macho yake kama mwali wa moto, na miguu yake mfano
wa shaba iliyosuguliwa sana.*

Nayajua Matendo yako . . .

128 Unaona, yote inakuwa ni matendo sasa, unaona, kwa sababu huyo ndiye anayempanda.

. . . na upendo na huduma, (unaona, yote ni ninii tu . . .) na mani na subira yako; tena kwamba matendo yako (tena, mara mbili, "matendo yako") ya mwisho yamezidi yale ya kwanza.

129 Unaona, hilo linaonyesha ya kwamba, Wakati wa Thiatira, baada ya mpinga-Kristo kutulia na kuingia katika Wakati wa Thiatira, hilo Kanisa dogo halingefanya kitu ila—ila kufanya kazi tu.

130 Na jambo lingine, ndama ni, pia, ni Mnyama wa dhabihu. Mnaona? Wao wanatoa maisha yao tu bure kama walivyoweza kuyatoa, katika zile nyakati za giza, miaka elfu moja kule ambapo Ukatoliki uliutawala ulimwengu. Nao waliingia tu moja kwa moja, ndiyo ama siyo. Wao hawakujali kufa. Kama ilikuwa ni mauti, hilo ni sawa. Wao walienda na wakafa, hata hivyo. Kwa nini? Roho yenyewe hasa ya wakati huo!

131 Hiyo ndiyo sababu hao, hiyo ndiyo sababu ya Ireneo, hiyo ndiyo sababu ya Polikapu, Yohana, Paulo, hao watu wakuu na hodari, walipigana na kitu hicho!

132 Paulo alikiona kitu hicho. Alisema, "Ninajua, ya kwamba baada ya kuondoka kwangu, ya kwamba mbwa mwitu wataingia miongoni mweni, enyi ndugu, wakifundisha mambo ya upotovu, na jambo hilo litawapotosha." Mwangalie maskini mtume huyo thabiti, akisimama pale, mgongo wake umepigwa ukajaa majeraha ya mijeledi, macho yake yakitoka maji. Lakini yeye aliweza kuona mbali kuliko ninii yao . . . ile darubini inayoangalia mbali sana kule ng'ambo, hivi kwamba wao wanaweza kuona umbali wa miaka mia moja na ishirini ya anga la nuru. Yeye aliweza kuona moja kwa moja mpaka Umilele. Huyu hapo. Naye alibashiri jambo hilo na kusema ya kwamba hilo ndilo litakalotukia. Na akasema, pia, akaendelea hata kwenye ule wakati mwingine ujao. Sasa angalia, ilikuwa ndiye yeye hapo.

133 Kisha, baada yake, Yohana Mtakatifu aliishi muda mrefu kuliko wote. Na wakati Yohana Mtakatifu alipokuwa akijaribu kuchukua nyaraka zote takatifu, akiwa ametiwa mafuta na Roho Mtakatifu, na kuziweka pamoja na kufanya Biblia, dola ya Kirumi ilimkamata na kumweka kwenye Kisiwa cha Patimo. Alikuwa kule nje kwenye Kisiwa cha Patimo kwa ajili ya Neno la Mungu. Polikapu alikuwa anamsaidia kuitafsiri.

134 Nilisoma, juzijuzi, barua ambayo Mariamu mwenyewe alimwandikia Polikapu. Na kumkemea . . . si kumkemea. Lakini kumpongeza kwa ajili ya kuwa mtu hodari kwamba ambaye angefundisha na kuyakubali mafundisho ya Yesu Kristo, Ambaye alizaliwa naye, kutoka kwa Mungu. Barua ya Mariamu mwenyewe aliyomwandikia Polikapu.

135 Polikapu alilishwa kwa simba, mwajua. La, yeye alichomwa moto. Mu—muda ulikuwa umeenda sana kwao kumfungulia simba kwenye uwanja wa michezo, na kwa hiyo walibomoa bafu, chumba cha bafu pale cha zamani, na kumweka kwenye—kwenye uwanja wa michezo na—na kumchoma moto.

136 Na alipokuwa njiani akienda, akishuka, alikuwa akienda huku ameinamisha kichwa chake. Jemadari wa Kirumi akasema, “Wewe ni mzee, na unaheshimiwa sana. Kwa nini usikane kitu hicho?”

137 Yeye alikaza tu kuangalia Mbinguni. Ndipo Sauti ikanena kutoka mahali fulani. Wao hawakuweza kufahamu ni wapi. Ikasema, “Polikapu, usiogope. Niko pamoja nawe.” A-ha. Kwa nini? Yeye alikuwa amesimama na hilo Neno.

138 Na wakati walipoanza kulundika mbao juu yake, wamchome moto, kulishuka muziki wa Kimbinguni. Na—na nyimbo za furaha kutoka kwa Malaika fulani mahali fulani zikaimbwa. Yeye hata mara mmoja hakuwapepesea jicho hao wenye kudhihaki.

139 Hao ni watu hodari. Hao ni watu ambao wanaweza kusimama. Hao wafia imani kote katika zile nyakati, kule, waliteseka sana. Lakini wao walikuwa nini? Walikuwa chini ya upako, Roho wa Mungu, zile nguvu. Mimi . . .

140 Msisahau jambo hili, enyi kanisa. Na ninyi ndugu, mlio kwenye kanda, ninataka mwangalie jambo hili kwa makini. Watu wangewezaje kufanya jambo lingine mbali na nguvu za Mungu ambazo zimeachiliwa kwao? Nitaliweka sanduku hili hapa juu, kuwakilisha jambo hilo. Kama Mungu akimtumia Roho fulani miongoni mwao, hicho ndicho kitu pekee wanachoweza kutenda kazi nacho, ni Roho anayetenda kazi miongoni mwao. Sasa tutawathibitishieni, kwa historia ya Kanisa, na kwa—kwa kufunuliwa kwa ile Mihuri, na zile nguvu zilizoachiliwa; na mwangalie, sawasawa kabisa, Kanisa liliupokea ule—ule upako, na hawakuweza kufanya jambo lingine lo lote.

141 Sasa, wa kwanza alikuwa ni yule simba aliyenguruma, lile Neno safi, lisiloghoshiwa.

142 Wa pili, katika Thiatira, alikuwa ni yule ndama. Na alikuwa ame—amebeba mzigo . . . Mnyama wa kuchukua mizigo. Samahani. Na pia alikuwa ni Mnyama wa dhabihu. Na hilo si lilikuwa kweli ni maskini Kanisa lile dogo? Rumi ilikuwa imetulia kule, katika miaka elfu moja ya nyakati za giza, na

cho chote ambacho hakikukiri kuwa ni cha kanisa la Kirumi kiliuawa mara moja. Nao iliwabidi kufanya kazi, kwenda mahali hadi mahali.

143 Ninyi Wamasoni, nitawakumbusha. Mnakumbuka ile ishara ya msalaba? Sasa, m—mnajua ninalozungumzia.

144 Sasa angalieni. Sasa, kama mki—kama mkiangalia, huko kulikuwa ni kuweka na kuihifadhi ile Biblia. Mnaona? Nao iliwabidi kufanya kazi miongoni mwao. Haya basi, ndama. Na wakati ulipowadia . . . Tulisoma jambo hilo jana usiku. Mnaona, wakati kitu hicho kilipotoka kwenda, na ile dhabihu ikaja, nao iliwabidi waende.

Yeye alisema, “Usidhuru divai na Mafuta.”

145 Wao walifanya nini? Walienda kule kwa hiari yao na wakafa. Hawakujali, kwa sababu Roho ya Kanisa ya siku hiyo ilikuwa ni ya kujitolea, kazi. Nao walienda kule kwa hiari yao tu walivyoweza, wametiwa upako na Roho wa kweli wa Mungu wa wakati ule, nao wakafa kama mashujaa, dhabihu; maelfu mara elfu, milioni sitini na nane wa hao kwenye kumbukumbu.

146 Ndama, dhabihu! Loo! jamani! Mnaelewa na jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina”—Mh.] Sawa. Vema. Sasa, dhabihu, wao wangeweza tu kuchapa kazi katika wakati huo, kuupinga ule upinzani mkuu katika miaka ile elfu moja.

147 Sasa, yule mnyama wa tatu aliyenda toka kwa Ibilisi, alikuwa ni huyu farasi mweusi. Unaona?

148 Sasa, Mnyama wa tatu aliyetoka, nguvu fulani kutoka kwa Mungu, kukabiliana naye, kukabiliana na nguvu za huyo mpanda farasi mweusi; alikuwa ni mwanadamu, mjanja, mwerevu, akiwa na hekima ya Mungu. Unajua, mwanadamu ndiye mwenye akili zaidi, kuliko wanyama wo wote wale. Unaona? Yeye ana akili zaidi, maana anaweza kumshinda kwa akili, kabisa kwa ujumla. Yeye ni mjanja, mwerevu. Unaona? Naye . . .

149 Ule—ule wakati, kutoka ule wakati wa giza, sasa tukitoka kwenye ule wakati wa giza; sasa, upande huu mwingine, wakati huyu mpanda farasi mweusi alipokuwa anaenda, walipotozwa dhabihu za—za—za—za na kila kitu walichofanya. Na pesa zilikuwa tu . . . Loo! unajua jinsi ilivyokuwa.

150 Sasa, kitu kingine kilichotoka kwenda, kukabilina na kitu hicho, ilikuwa ni yule Mwenye Uhai mwenye uso kama wa mwanadamu; mwenye akili, mwenye elimu, mwerevu, stadi, aliyetiwa upako na Roho huyo wa siku hiyo. Unaona jambo hilo? Sasa, yeye alienda kukabiliana naye, na ujanja wa hekima ya Mungu aliyokuwa nayo. Huo ulikuwa ni ule wakati wa matengenezo, Martin Luther, John Wesley, na kadhalika. Unaona, ilikuwa ni yale matengenezo. Zwingli, na, loo! nani wengine wote, Knox, Calvin, na nani wengine wote, unaona,

waliotoka. Ulikuwa ni ujanja. Sasa, wewe angalia, kutoka kwenye wakati wa giza hasa, kutoka kwenye yale matengenezo, kuja upande huu mwingine, angalia, ilikuwa ni busara ya mwanadamu.

151 Laiti mngaliweza kufungua madirisha yenu kidogo tu! Ninadhani watu wanapata joto kidogo, naam, labda, kule ndani. Kama mngevuta madirisha chini kidogo. Maana, ninajua, iwapo mimi ninayesimama hapa nikihubiri, ninapata joto, ninajua hamna budi mnalipata huko mliko.

152 Vema, angalia, ilikuwa ni busara ya mwanadamu. Sasa, mnaelewa?

153 Huyu mnyama wa tatu aliyetumwa na Shetani, akawa mwerevu, pia. Angalia, “Kibaba cha ngano kwa nusu rupia. Vibaba vitatu vya shayiri kwa nusu rupia.” Unaona? Loo! jamani! Unaona? Ile njama ya kupata pesa, ule ujanja, kupata dhahabu ya dunia, na utajiri, viingizwe kwake. Hilo linatimiza kabisa. Hiyo ndiyo sababu kuanza kutoza pesa kwa ajili ya maombi. Na kwa . . . Akabuni mahali panapoitwa pergatorio, na kuwaombea mababu zao watoke huko. Na, loo! ilikubidi kutoa hati-miliki zako na kila kitu, mali yako. Kanisa, na lilikuwa taifa, vilikuwa kitu kimoja, nalo kanisa lilichukua mali yako.

154 Nanyi hamwoni, baadhi ya hawa wainjilisti, siku hizi, wangali wana upako uo huo juu yao? Wakiwafanya wazee watoe pesa zao za kustaaifu, na kutoa hati-miliki za nyumba zao kwa ajili ya mambo fulani. Mbona, ndugu, si—sitaki kuingilia jambo hilo, unaona. Lakini sasa nitadumu moja kwa moja na jambo hili; mimi ninaangalia nyuma kuona ninakoelekea. Sasa angalia, hao watu, hiyo ni juu yao. Hilo ni juu yao. Hilo—hilo—hilo halina uhusiano wo wote na mimi. Mimi ninawajibika tu kwa Hili hapa.

155 Sasa angalia, yule—yule Mnyama aliyekuwa kukabiliana naye, sasa, alikuwa ni mwanadamu. Nasi sote tunajua ya kwamba Mnyama huyu, wa mwanadamu, nguvu hii ya mwanadamu, katika akili zake, ilitambua ya kwamba ule mkate mwembamba ambao Martin Luther alikuwa ameushika mkononi mwake, wakati alipokuwa akipanda vile vipandio . . .

156 Wao walisema, “*Hii* ni Damu ya Yesu Kristo. *Huu* ni mwili wa Yesu Kristo.”

157 Na Luther akautupa chini, na kusema, “Ni mkate na divai. Si mwili wa Kristo; maana, umetukuzwa, na unaketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu, akituombea.” Unaona, hekima; unaona, mwanadamu.

158 Na wakati John Wesley alipokuja, baada ya Zwingli kuingia, na Calvin.

159 Nao wakalifikisha kanisa mahali, kwenye usalama, mpaka hawakutaka miamsho mingine. “Lo lote litakalotukia litatukia.” Ni hayo tu. Nao waliishi maisha ya namna yo yote. Kanisa la

Kiluteri limechanganyikiwa sana, na kanisa la Anglikana! Loo! jamani! Nchi nzima ikawa imeharibika, kama tu ilivyo sasa. Makanisa yalikuwa yamechanganyikiwa. Wakati Mfalme Henry wa—wa VIII, alipokuja Uingereza, na baada ya mwuaji Mary, na mambo haya yote kutokea. Na, basi, kanisa lilikuwa limejaa ghasia nyingi na machafuko. Wengi wakidai Ukristo, na huku wanaishi na wake wanne ama watano, ama wakifanya jambo lo lote walilotaka kufanya, na kufanya yasiyofaa, na unajisi.

¹⁶⁰ John Wesley, akiyasoma Maandiko, akiangalia jambo Hilo, alifunuliwa ya kwamba Damu ya Yesu Kristo humtakasa mwamini. Nawe unaninii . . . haikupasi . . . Ndipo alifanya nini? Yeye alitoka akaenda akafanya matengenezo mengine. Aliuokoa ulimwengu katika siku yake, kama Luther alivyofanya. Unaona? Ilikuwa ni nini? Ni mtu huyo, zile nguvu za Mnyama, zikitoka zikaenda.

¹⁶¹ Akampa mwanadamu hekima, ya kufahamu, ya kwamba kitu hicho ni kibaya. “Hiyo si Damu ya Yesu Kristo. Huo si mwi—mwili wa Yesu Kristo. Huo unawakilisha ule mwili.” Unaona?

¹⁶² Huo ungali bado ndio ubishi mkali kati ya Mkatoliki na Mprotestati sasa hivi. Hilo ndilo jambo la pekee hamwezi kupatana juu yake sasa hivi. Mengine yote, wanaweza kupatana, ila jambo hilo; kwenye mabaraza haya wanayofanya. Angalia sasa. Lakini, hili, lakini ha—hawangeweza kupatana katika jambo hilo. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara tatu—Mh.] Unaona?

¹⁶³ Mmoja, “Ni Damu, na,” anasema, “ni Damu halisi; eti kwamba kasisi ana mamlaka ya kubadilisha mkate huu uwe mwili halisi wa Kristo.” Ndio hicho kile kijisanduku kilichoko kule, ka—kanisani, unajua. Hiyo ndiyo sababu wanafanya alama na kila namna ya matoleo ya kipagani wanapopita hapo, mnajua, na kusujudu, na kuinamisha kofia zao, na kadhalika. Hiyo si kwa ajili ya lile jengo; ni kwa ajili ya huo mkate mwembamba ulio kwenye kile—kile kijisanduku. Basi angalia jinsi Shetani alivyoingiza hilo kwa hila!

¹⁶⁴ Lakini, unaona, wakati ule, ndani ya utu wa huyo mtu, unaona, Mungu aliweka Roho ya hekima juu ya binadamu, kufahamu ya kwamba jambo hilo ni makosa. Sasa, hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya kukabiliana na yule mnyama wa tatu, ambaye alikuwa amelipotisha kanisa sana, ambalo alikuwa akiendesha, mpaka likawa jambo la kuchukiza sana. Wale watengenezaji, walifanya nini basi, wao katika wakati wa watengenezaji? Walilirudisha Kanisa, kutoka kwenye ibada zake za kipagani za kuabudu sanamu, kulirudisha kwa Mungu tena. Unaona? Hiyo ndiyo sababu yule Mwenye Uhai alitoka, ile busara ya mwanadamu, yule mpanda farasi, kufanya jambo hilo.

¹⁶⁵ Sasa, lakini, soma sasa aya ya 3 na . . . ama, Ufunuo 3:2, kwa muda kidogo tu. Sasa, nimeliandika chini hapa kwa sababu

fulani. Sasa huu ni, unakuja sasa, wakati wa Waluteri, katika wakati wa watengenezaji, wa Ufunuo 3:2.

166 Walilofanya, waliunda madhehebu. Mara Luther alipoanzisha kanisa lake, wao walilifanya madhehebu. Vema. jambo lile lile alilofanya Wesley. Jambo lile lile walilofanya Wapentekoste, sawasawa kabisa, wakaunda madhehebu. Nao wanafanya nini? Wao wanachukua utaratibu ule ule wa kule walikotoka. Unaona?

167 Sasa angalia jambo hili, Ufunuo, ikinena juu ya kanisa hili la Sardi. “Kwa malaika wa kanisa,” ndiyo aya ya 1, bila shaka. Unaona? Vema.

Uwe mwenye kukesha, ukayaimarishe mambo yaliyosalia,

168 Hiyo ni kusema, “Neno ulilofundishwa,” unaona, “mambo yaliyosalia.”

. . . yanayotaka kufa . . .

169 Yeye wakati huo yuko tayari kurudi kwenye madhehebu kama tu lile kanisa Katoliki kule alikotoka. Unaona?

. . . maana sikuona matendo yako kuwa yametimilika mbele za Mungu.

170 Haya basi. Hiyo hapo ninii. . . Huyo hapo anaenda, anarudi moja kwa moja tena. Hivi huoni ni kwa nini taratibu za kimadhehebu si halali? Ni nani aliyezianzisha? Ni Mungu? Ni mitume? Kanisa la Romani Katoliki lilifanya jambo hilo. Sasa hebu mwanahistoria ye yote na aseme vinginevyo. Halipo. Wao ni, wao wanasema ati ndio kanisa mama, na ndiyo walivyo. Lakini walikifanya kitu hicho madhehebu, na kuweka utaratibu, wakaweka kiongozi wa kibinadamu juu yake. Nasi hatukumchukua mtu mmoja, kama wao walivyofanya; tunachukua halmashauri nzima ya wanadamu, tukawaweka pamoja, na halafu kweli una machafuko. Hiyo ni kweli. Halmashauri inawezaje, hata hivyo?

171 Ni kama vile tu, tunafikiri demokrasia ni kitu cha kweli. Ninaamini hivyo, pia, lakini haitafanya kazi sawasawa kamwe. Haiwezi. Kukiwako na kundi la akina Ricky hapa kuitekeleza, utawezaje kamwe kuifanya sawa? Huwezi. Angalia, jambo halisi lilikuwa ni mfalme anayemcha Mungu.

172 Angalia yule Mnyama, yule Mnyama wa tatu, sasa, alikuwa ni hekima ya mwanadamu. Naye aliwawakilisha wale watengenezaji waliotoka wakaenda.

173 Tokea kwenye sanamu, ya kuchukua, kusema, “*Huu ni mkate.*” [Ndugu Branham anapiga makofi mara nne—Mh.] “*Hii ni divai.*” [Ndugu Branham anapiga makofi mara mbili.] Unaona, mpinga Kristo angali bado ana kitu kinachowakilisha Ukristo. Hana budi kuwa nacho, maana yeye ni “mpinga,”

unaona. Na halafu basi, kama yeye hana budi kuwa anapinga kitu fulani. . .

174 Sasa, kama akija moja kwa moja, aseme, “Loo! mimi ni Mbudha.” Vema, hilo halina cho chote. Wote hufanya jambo hilo. Huyu ni kafiri tu, kwanza.

175 Lakini mpinga-Kristo ni mjanja. Yeye ana kila namna ya mambo yanayowakilisha Ukristo pale. Ni kwamba tu, aliyaweka upande ule mwingine, jambo fulani linalopinga Fundisho la asili la Jambo Lenyewe. Unaona, hilo ndilo linalomfanya mpinga-Kristo. Unaona?

176 Kwa hiyo, wale watengenezaji, wakati yule Mnyama alipotoka akaenda katika mfano wa—wa mwanadamu, kumkabili huyo!

177 Sasa, msisahau jambo hili, enyi darasa! Msilisahau [Ndugu Branham anapiga-piga mimbara mara nne—Mh.] Mnaona? Kumbukeni Hilo, siku zote za maisha yenu! Mnaona? Hawa Wenye Uhai ni sahihi. Ni BWANA ASEMA HIVI. Mnaona?

Angalia, ibada ya sanamu ilileta ninii. . .

178 Mwenye Uhai wa kibinadamu aliondoka akaenda akiwa na nguvu za Mungu, kwa hekima aliyopewa na Mungu, na kulitoa kanisa katika ibada ya kuabudu sanamu, akalirudisha kwa Mungu. Lakini katika. . .

179 Tunaona ya kwamba, katika wakati ule ule wa kanisa, wakati walipoanza kufanya madhehebu, kufanya jambo lile lile walilofanya hapo mwanzo, ambalo Roma ilifanya, sasa litalizalia kanisa hilo binti. Naye anasema nini?

180 Kasema, “Sasa kwa sababu unaninii. . .Sijakuona kwamba u mkamilifu. Na huna budi kuimarisha nguvu hiyo kidogo iliyosalia.” Sasa msikilize Yeye akiwaonya, katika Ufunuo tena, 3:3. Hebu tufungue. . . Vema, ninaamini nilipata, dakika chache tu zilizopita.

Basi kumbuka namna ulivyopokea, na jinsi ulivyosikia; yashike hayo na kutubu. . .

181 Ninii tu, kwa maneno mengine, “Kumbuka ulitoka katika upotovu kama huo.” Unaona? Pia angalia hapa.

. . . Walakini usipokesho, nitakuja kwako kama mwivi (a-ha), wala utajua. . . Wala hutaijua saa nitakayokuja kwako.

182 Na kuendelea, Yeye ataondoa hicho kinara cha taa, unaona. Kwa hiyo, jambo ndilo hilo. Ni kitu gani? Nuru ya Kanisa.

183 Nalo likaingia moja kwa moja kwenye utaratibu ule ule wa kimadhehebu wa giza la kipagani lilikotoka, na lingali limebakia huko leo, pamoja na watu wenye mioyo minyofu wakifikiri ya kwamba hilo ndilo la Kweli, kama vile tu Wakatoliki wanavyofikiria. Nao Waprotestanti wanawacheka

Wakatoliki; ambapo, wote ni kitu kile kile, hakika, kulingana na Neno. Hekima ya mwanadamu!

184 Sasa angalia. Loo! jinsi ninavyolipenda jambo Hili! Msikilizeni Yeye sasa akiwaonya. Sasa, sasa sisi... Mnakubaliana nalo kikamilifu, kila mmoja wenu? Sasa, kama hamkubali, niandikieni swali. Kwamba, hao Wenye Uhai tayari wametambulishwa kikamilifu katika kila wakati, kama vile Biblia iliwatambulisha hapa. Hivyo ndivyo walivyofanya pale hasa. Historia inaonyesha yale waliyofanya. Tunaangalia papa hapa na kuona yale waliyofanya.

185 Na hapa, hao Wenye Uhai, si—si—sikujua jambo hilo hapo siku za nyuma. Nilikuwa nimeketi tu pale. Niliweza kuliona tu likitendeka pale, kama tu vile mnavyoniangalia mimi. Mnaona? Na halina budi kuwa sahihi, maana liko papa hapa kwenye Biblia. Kwa hiyo sasa utaenda kufanya jambo gani lingine gani ila kusema ni kweli? Angalia.

186 Sasa, yule Mwenye Uhai wa nne, aliyetumwa kukabiliana na mpinga-Kristo, katika Mwenye Uhai huyu wa mwisho. Mko tayari? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yule Mnyama wa mwisho aliyetumwa, ama ile nguvu ya mwisho ya kumpinga mpinga-Kristo ambaye alikuwa anapingana na Mafundisho ya Mungu, yule mpinga-Kristo, alikuwa ni tai. Mnaona? Yule Mwenye Uhai wa nne alikuwa ni tai. Sasa, someni tu zile nyakati, someni Maandiko. Ni tai! Na katika Biblia, wakati wa mwisho ulikuwa ni wakati wa tai. Na Mungu humlinganisha tai na manabii Wake. Unaona? Ni... Sasa angalia. Wakati wa mwisho, ule wakati wa tai, m—mfunuzi wa Neno la kweli. Unaona?

187 Kabla Mungu hajatenda jambo, kama alivyofanya katika siku za Nuhu, Yeye alimtuma tai. Wakati alipomleta Israeli, na jeshi la Farao lilipokuwa tayari kwenda, Yeye alimtuma tai. Kila wakati, Yeye humtuma tai mwishoni, mwisho wa jambo hilo.

188 Na hapa Yeye anamtuma tai, tena. Hilo ni kulingana kabisa na Neno. Kwa hiyo unawezaje kulifanya liwe kitu kingine kile? Yeye humtuma tai, (kwa nini) mfunuzi wa ile Kweli ambayo imekuwa ikishuka wakati wote katika wakati huo.

189 Kwa hiyo inawezekanaje hata kidogo kwa nda—ndama, ama ninii—ama mwanadamu, ama Mnyama ye yote aliyekuwa amepanda farasi, lingeweza kufunuliwa mpaka atakapokuja tai? Wao walikuwa na mahali pao; walikuwa ni Wenye Uhai watauwa, waliotumwa, kama tu vile mtu mwingine ye yote alivyokuwa.

190 Simba, huyo alikuwa ndiye wa kwanza. Hapo ndipo mpinga-Kristo alipotokea vi—vitani.

191 Ndipo akainua nguvu nyingine; Yeye akatuma nguvu fulani kuikabili.

192 Kisha akainua nguvu nyingine; Yeye akatuma nguvu nyingine kukabilihana nayo.

193 Na ndipo kwenye ile nguvu ya mwisho, Yeye anamleta tai, “Kuwarudisha watoto kwenye ile Imani ya asili tena, ya baba zao.” Wakati wa tai! Halafu, kama ukiangalia, hakuna Wanyama wengine tena. Wamekwisha. Huo ndio mwisho. Sasa, kama ungechukua sasa Ufunuo 10:1,7. Nimekuwa nikitaja hiyo. Kumbuka, katika wakati wa mjumbe wa mwisho, unaona, nini kilichokuwa kitukie? “Siri zote za Mungu zingefunuliwa.” Yule tai! Amina!

194 Sasa unaona wale wanyama wanne walioendeshwa. Hilo lilikuwa ni sawa kamilifu kabisa. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.” Mh.] Na sasa kila wakati uko hapa, ama kila nguvu ambayo iliandamana nao. Na hayo ndiyo Maandiko yanayoonyesha yale aliyofanya adui mpanda farasi. Mambo hayo yamefunuliwa katika Mihuri hii. Na pia imefunuliwa sasa ya kwamba kila Mwenye Uhai, nguvu aliyotuma Mungu, kukabilihana naye, inalingana kikamilifu kabisa, hata kufikia wakati wa tai. Sasa, kama huu ndio wakati wa mwisho, atakuja tai, kweli, na ni kwa ajili ya jambo hilo. Sasa, mkumbuke.

195 Sasa, katika siku ambazo simba alikuja, lile Neno la asili, waliomsikiliza simba ni kama moja juu ya mia.

196 Katika siku ambazo nda—ndama alikuja, ni tone dogo sana la hao lililousikiliza ujumbe wa ndama.

197 Katika siku ambazo mwa—mwanadamu alikuja, alitenda kazi kati ya wanadamu, unaona, kwa hiyo Yeye alikuwa na busara. Alitoa kundi dogo.

198 Nao walifanya nini? Shetani aliona jambo hilo, kwa hiyo yeye anawarudisha moja kwa moja na kuwaoza kwenye jambo hilo.

199 Basi kumbukeni, wakati hatimaye tai atakapokuja, itakuwa ni moja ya mia ya asilimia mia moja watakaosikiliza. Ni wakati wa tai. Kumbukeni, ni hawa wapanda farasi wengine wote. . . Na halafu hata Yesu alibashiri, “Kama Yeye hakuharakisha Kuja Kwake, hakungekuwa na mwenye mwili ye yote, kamwe, angeokolewa kwa ajili ya Kunyakuliwa.” . . .? . . . Hayo ni Maandiko? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaona mahali tulipo sasa, sivyo, ndugu na dada? [“Amina.”] Mnaona mahali tulipo?

200 Mungu, ninafurahi sana, si—si—sijui la kufanya! Huyu si mimi ninayesimama hapa ku—kuzungumza. Niko hapa ndani, pia. Mimi, niko miongoni mwenu. Mnaona, mimi, ni mimi. Nina familia. Nami nina ndugu na dada ninaowapenda. Na Mungu wa Mbiguni, akiwa ni mwema sana kushuka na—na kufunua jambo hilo, kwa njia ya watu Wake, kwa maono ambayo yamethibitishwa kwa muda wa miaka thelathini, kuwa ni ya Kweli. Tumewasili. Tumeninii. . . Tumewasili. Hakuna cha zaidi

tena. Utafiti wa kisayansi umethibitisha jambo Hilo. Thibitisho la Neno limehakikisha jambo Hilo. Nasi tumewasili! Na ufunuo huu unatoka kwa Mungu, nao ni Kweli!

²⁰¹ Mmeshika jambo lo lote? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Nilijiuliza tu kama mmeshika kitu. Unaona? Naam, bwana. Huenda haitanilazimu kuwaambia wakati huo basi, Jumapili. Angalieni. Angalieni. Ni ajabu! Sasa, sasa, angalieni sasa.

²⁰² Na halafu kulingana na—na wakati ambao Mungu alikuwa akienda kuukomboza ulimwengu uliotangulia ile gharika, Yeye alimtuma tai.

Na wakati alipokuwa akienda kuwakomboza Israeli, alimtuma tai.

²⁰³ Je! mnaamini ya kwamba wakati, hata kwa Yohana, kwenye Kisiwa cha Patimo, Ujumbe huu ulikuwa ni mkamilifu sana hata hangeweza kuuweka mikononi mwa Malaika? Mnajua, malaika ni mjumbe. Lakini je! mnajua yule mjumbe alikuwa ni nabii? Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.—Mh.] Hebu na tulithibitisho hilo. Ufunuo 22, hebu na tuone kama alikuwa ni tai. Naam. Mnaona, yeye alikuwa nanii... Hakika, alikuwa ni malaika, ndiye yule mjumbe, lakini nabii ndiye aliyekifunua Kitabu hiki chote cha Ufunuo kwake.

²⁰⁴ Ufunuo, mlango wa 22 na kifungu cha 19, ninaamini hiyo ni kweli kama nimeliandika hapa... 22:19, huenda nimekosea. La. [Mtu fulani anasema, “Ni 22:9, labda.”—Mh.] 22:9, ndipo penyewe. Nilikuwa nikiangalia 22:9. Hiyo ni kweli. Loo! ndio, hapa.

Naye akaniambia, Angalia, usifanye hivi; maana mimi ni wajoli wako, na wa ndugu zako manabii,...

²⁰⁵ Angalia yale Yohana aliyoona hapa.

...Nami Yohana ndimi niliyeyasikia na kuyaona mambo haya.

²⁰⁶ Sasa yeye anafunga. Hii ni sura ya mwisho.

...Na hapo ni...nilipoyasikia na kuyaona nalianguka, ili nisujudu mbele ya miguu ya malaika yule Mwenye kunionyesha mambo haya, mwenye kunionyesha mambo haya.

²⁰⁷ Na, “yeye,” basi, “yule malaika,” mnaona.

Naye akaniambia, Angalia, usifanye hivi;...

²⁰⁸ Hakuna nabii wa kweli angeabudiwa, au mjumbe wa namna yo yote, unaona. Huko ni kwa Mungu peke yake.

Naye akaniambia, Angalia, usifanye hivi; kwa maana mimi ni mjoli wako, na wa ndugu zako manabii, na wa wale wayashikao maneno ya kitabu hiki. Msujudie Mungu.

209 Unaona? Sasa, kile Kitabu kilikuwa ni muhimu sana, kwamba, ni Neno la Mungu. Sasa angalia. Na wakati Neno la Mungu linapoletwa, halina budi kuletwa na nabii, kwa maana huyo ndiye anayejiliwa na Neno la Mungu.

210 Nilikuwa nikitarajia kupata swali juu ya jambo hilo, katika—katika sanduku hili hapa. Nilifikiri ningewatangulia, kidogo, wajua. Ninahisi tu kuna moja pale ndani la namna hiyo, ni hayo tu. Ni—nilidhani tu ningelifikia, unaona. Unaona?

211 Kila Neno la Mungu huletwa. Biblia haibadilishi utaratibu, hata kidogo, unaona. Ni jambo lile lile. Halina budi kumjia mwonaji huyu tunayemtarajia kufika, sasa angalia, Ufunuo 10:1,7.

212 Sasa hebu na tusome ki—kifungu cha 9 tena. Sasa tunapata . . . sisi . . . Sasa, kabla hatujaiendea ile aya, ninataka kuwaulizeni jambo fulani.

213 Mnaona, vizuri kabisa, kabla hatujaiacha Mihuri hii? Sasa kumbukeni, hakuna nguvu nyingine zinazotoka kwenda baada ya huyo tai, unaona, hakuna tena. Kila wakati mpinga Kristo alipotuma kitu fulani, Mungu alituma nguvu fulani. Mpinga-Kristo akatuma nguvu nyingine; Mungu akatuma kitu fulani cha kukabiliana nayo. Kisha akatuma nguvu nyingine; Mungu akatuma kitu fulani kukabiliana nayo. Unaona? Na basi wakati alipofika kwa yule tai, hilo ilikuwa ni Neno Lake, likirudi kama lilivyokuwa pale mwanzo.

214 Sasa angalia. Je! yule nabii tunayemtarajia aje, si ni mtu fulani aliyetiwa mafuta na—na Roho kama Eliya? Haitakuwa ni Eliya, bila shaka. Lakini itakuwa ni mtu fulani, wa namna hiyo, atakayeshuka. Na huduma yake hasa ni kutuma, kuwarudisha, watu hawa walioanguka waliomo kwenye madhehebu haya yaliyopotoka, kurudia kwenye Imani asili ya baba zao. Sasa, kama hilo haliifungamanishi Biblia hiyo pamoja, si—sijui ni kitu gani kinachoifungamanisha. Si—si—siwezi kusema zaidi juu ya jambo hilo, maana ndio hilo. Mmeshawasili sasa hivi tu. Hiyo ni Kweli. Ukiondoa jambo lo lote kutoka hapo, unalipotosha. Unaona? Kwa hiyo, hilo, halina budi kuwa namna hiyo tu.

215 Sasa angalia, sasa, katika aya ya 9, “Roho zilizo chini ya madhabahu.” Sasa, hapa ndipo nitakapoenda kupata upinzani kwelikweli. Lakini hebu angalieni tu kwa muda kidogo. Na hebu ninii tu. . . Unaona? Nilifikiria jambo hilo, pia, lakini halikuja namna hiyo. Tuna . . . Daima nimewaza ya kwamba roho hizi chini ya madhabahu zilikuwa ni wale—wale—wale wafia imani wa Kanisa la mwanzoni. Nami nina hakika ya kwamba Dk. Uriah Smith, na kila mmoja wao, anasema ndio. Mnaona? Lakini, nilifikiria hivyo, mimi mwenyewe. Lakini wakati Roho Mtakatifu aliponionyesha ono lake, haikuwa hivyo, si zile roho.

Sasa, sasa unasema, “Vema, lakini, mimi silioni jambo hilo.”

216 Vema, sasa, hebu kidogo, tutaona. Angalia. Hizi si roho za—za Kanisa la Bibi-arusi, hata kidogo. Tulifikiri hilo lilikuwa ni Kanisa la Bibi-arusi linalongojea kule, roho chini ya madhabahu, unaona, zikilia, “Hata lini, Bwana, hata lini?” Hebu nilisome tena sasa, ili tulipate barabara.

Na alipoifungua muhuri ya tano, nikaona chini ya madhabahu roho zao waliochinjwa kwa ajili ya neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao.

217 Unaona, “Neno la Mungu, na ushuhuda waliokuwa nao.” Sasa, msi—msiondoke hapo. Ngojeni kidogo, unaona.

Wakalia...Ee Mola, hata lini?... (mnaona?)... Mtakatifu, Mwenye kweli, hata lini...kutokuhukumu, wala kuipatia haki damu yetu kwa hao wakaao juu ya nchi?

Nao wakapewa kila mmoja nguo ndefu, nyeupe, wakaambiwa wastarehe bado muda mchache, hata itakapotimia hesabu ya wajoli wao na—na ndugu zao, . . . watakaouawa vile vile kama wao.

218 Sasa, kwa kuwa wao, wakati huu, kama ukiangalia, huu Muhuri wa Tano ukifunguliwa, unaona, Kanisa limekwisha ondoka. Haiwezekani tu kabisa, roho chini ya—lile Kanisa la mwanzoni.

219 Sasa, sasa, tafadhali, kama ulipata kulisikiliza jambo hili kwa makini sasa, maana huu ndio ubish- . . . ubishi mkubwa, kwa hiyo nawatakeni msikilize kwa makini sana sasa. Na mna makaratasi yenu, na vitu vya kuandikia. Sasa, nawatekeni mwone.

220 Sasa, hizi haziwezi kuwa ni hizo roho. Maana, ro—roho za—za wenye haki, wafia imani, na watu wenye haki, Kanisa, Bibi-arusi, tayari zimenyakuliwa, kwa hiyo hawangekuwa chini ya madhabahu. Watakuwa Utukufuni, pamoja na Bibi-arusi. Sasa angalia. Kwa kuwa, wamekwenda katika ule Unyakuo, katika mlango wa nne wa Ufunuo. Walitwaliwa juu.

221 Sasa, hizi roho ni akina nani, basi? Hilo ndilo jambo linalofuata. Ni akina nani, basi, kama wao si kile Kanisa la mwanzoni? Hawa ni Israeli ambao wataokolewa kama taifa, wote ambao wamechaguliwa tangu zamani. Hao ni Israeli. Hao ni Israeli, wenyewe.

222 Unasema, “Loo! ngoja kidogo.” Unasema, “Haiwezekani kuwa ni wao.” Loo! naam, wao wataokolewa.

223 Hapa, hebu na tulitatie, dakika moja. Nina Maandiko manne ama matano. Nitachukua moja. Hebu na tuchukue Warumi, dakika moja, tuone kama ndio wao. Hebu tuchukue Kitabu cha Warumi, na twende kwenye—kwenye sura ya 11 ya Warumi, nasi tutaona. Ninii tu . . . Hebu na tulisome tu, na ndipo

tatalipata sisi wenyewe binafsi. Warumi, sura ya 11, aya ya 25 na 26. Sasa msikilizeni Paulo hapa.

224 Basi Paulo alisema, “Kama mtu mwingine ye yote, hata Malaika, akihubiri injili nyingine yo yote,” (ati nini?) “alikuwa alaaniwe.” Angalia.

Kwa maana, ndugu zangu, sipendi msijue siri hii, (aha), ili msijione kuwa wenye akili (naam); ya kwamba kwa sehemu ugumu umewapata Israeli, mpaka utimilifu wa Mataifa uwasili.

225 Yule Bibi-arusi Mmataifa wa mwisho aingizwe, kama Bibi-arusi, upofu uliwajia Israeli kwa kusudi hili.

Hivyo Israeli wote wataokoka; kama ilivyoandikwa, Mwokozi atakuja kutoka Sayuni; Atamtenga Yakobo na maasi yake.

226 Kweli! Sasa, wao ni Israeli, walio chini ya hii madhabahu. Angalieni. Israeli walipofushwa kwa kusudi hasa la sisi kuokolewa. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa, ni nani aliyewapofusha? Mungu. Mungu aliwapofusha watoto Wake Mwenyewe.

227 Si ajabu, Yesu, akiwa amesimama pale msalabani, na hao Wayahudi wakiililia Damu Yake! Hao walikuwa ni watoto Wake Mwenyewe. Naye alikuwa ndiye Maandiko. Alikuwa, Yeye Mwenyewe, ni Neno. Na hapa, Yeye akijua ya kwamba watu hao wanalimpokea Yeye Kwa furaha! Na hiyo ndiyo sababu Yeye aliwapofusha, ili kwamba wasimtambue. Yeye alikuja kwa njia ambayo ni nyenyekevu sana, na akawapofusha kwa hilo, ili kwamba wasiweze kumpokea. Unaona? Maandiko yalisema wao wangepanya jambo hilo. Naye aliwapofusha. Walipofushwa! Yesu aliwahurumia, hata kiasi, kama alivyosema, “Baba, wasamehe. Hawajui watendalo.” Unaona? Wao walikuwa vipofu. Paulo alisema walipofushwa kwa sababu fulani, kwa ajili yetu.

228 Angalia. Sasa ninawatakeni mwangalie jambo hili kwa makini sana. “Wakapewa nguo ndefu.” Wao hawakuwa nazo. Walipewa nguo ndefu, nguo ndefu nyeupe, kila mmoja wao. Sasa, watakatifu wanazo sasa, tayari wanazo; wanazipata hapa. Lakini, pale, “Wakapewa nguo ndefu.” Nao watakatifu tayari walikuwa na zao, na wameondoka. Unaona? Unaona? Wao walikuwa—hawakuwa. . .

229 Wao, unaona, hawakuwa na nafasi, kwa maana walipofushwa na Mungu, Baba yao Mwenyewe; ili kwamba neema ya Mungu ingeweza kutimizwa, ili kwamba Bibi-arusi apate kuchukuliwa kutoka kwa Mataifa. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

230 Hebu—hebu niwaonyeshe mfano mzuri hapa katika Yusufu; Yusufu, yule mtu wa Roho, yule tai. Alizaliwa kati ya ndugu zake, kama tu vile Kanisa halisi lilivyo miongoni mwa yale

mengine. Naye aliweza kutafsiri ndoto na kuona maono. Na hao wengine walimchukia. Baba yake alimpenda.

²³¹ Angalieni, basi, yeye alitoka, alifukuzwa na ndugu zake, hakufukuzwa na baba yake. Alifukuzwa, na ndugu zake, naye akauzwa kwa karibu vipande thelathini vya fedha. Akatupwa shimoni, na akadhaniwa kuwa amekufa.

²³² Akakwezwa, na akaketi mkono wa kuume wa Farao. Na kwa sababu alifukuzwa na ndugu zake, unaona, alipewa Bibi-arusi Mmataifa, si wa watu wake mwenyewe. Kwa njia hiyo, akamzaa Efraimu na Manase, ambao wajumlishwa katika Israeli.

²³³ Wakati Israeli alipokuwa anawabariki, kwa kupitanisha mikono yake, kutoka kwa aliye mdogo kwenda kwa aliye mkubwa, kupitisha baraka kutoka kwa Myahudi, kuzirudisha. . . ama kutoka kwa Myahudi kwenda kwa Mmataifa. Unaona? Alipitanisha mikono yake, kwa mwanawe mdogo, ambaye ni lile Kanisa changa litakalokuja. “Ka—kanisa mama lilisimama kwenye jua; likamzaa mtoto huyu mchanga.” Pia angalia, ili aweze kumpata, Israeli alipitanisha mikono yake, katika mfano. Naye Yusufu. . .

Watoto wao hao, walikuwa na mama Mmataifa.

²³⁴ Bibi-arusi wa Israeli, kule nyuma, akawa amepitanishwa, kutoka Orthodoxi ya kale, kuingia katika njia ya Ukristo, kwa Roho Mtakatifu aliyeipitanisha mikono ya Israeli. Yeye akasema, “Mungu ameipitanisha mikono yangu.” Hakuhusika na kulitenda jambo hilo.

²³⁵ Angalieni. Ndipo, Yusufu, akiwa amekataliwa na ndugu zake wenyewe, watu wake mwenyewe, akachukua Bibi-arusi Mmataifa. Vile vile kabisa Yesu alivyofanya; alipokataliwa na Wayahudi, akachukua Bibi-arusi Mmataifa

²³⁶ Sasa hebu na tusome jambo fulani hapa. Nina Maandiko yaliyoandikwa, Matendo 15. Na, loo! hili kwa namna fulani ndilo jambo tunalopaswa kufundisha, hata hivyo. Sasa, ninaamini nimelipata hili sahihi, someni Matendo 15:14. Vema. Ninatumaini hili ni sahihi sasa. Vema. “Simeoni ametueleza jinsi Mungu. . .” La, hebu tuanzie kwenye aya ya 13.

Na hao walipokwisha kunyamaza Yakobo akajibu, . . .

²³⁷ Sasa, mnaona, yale yaliyokuwa yametukia, walikuwa wamewaendea Mataifa. Mnaona? Ndipo ugomvi ukazuka, maana wao walikuwa ni Wayahudi. Mnaona?

Na hao walipokwisha kunyamaza Yakobo akajibu, akisema, Ndugu zangu, nisikilizeni.

Simeoni (huyo ni Simoni Petro) ametueleza jinsi Mungu hapo kwanza alivyowaangalia Mataifa ili achague watu katika hao kwa ajili ya Jina Lake.

238 A-ha! Unaona, jina la mke wangu lilikuwa ni Broy. Nilipomchukua, yeye akawa Branham. Unaona?

239 Yesu analitoa Kanisa Lake, ama Bibi-arusi Wake, kutoka katika Mataifa. Ni Maandiko, yakionyeshwa katika kivuli, kama tu ilivyokuwa kwa Yusufu.

240 Sasa angalia jambo hili, sasa, roho hizi chini ya madhabahu. Vema, ninii . . . hii, "Hizi roho," tukifahamu sasa, "ambazo ziko chini ya madhabahu," ni kwa nini ziliuawa na watu wenye dhambi kama Eichmann. Unaona? Wao wanashikilia moja kwa moja, mamilioni yao, unaona, lakini wao wanabakia kuwa Wayahudi.

241 Sasa, kumbukeni. Ilikuwa ni kitu gani? "Waliuawa kwa ajili ya Neno la Mungu," si kwa ajili ya ushuhuda wa Kristo. Hivi mlipata kufahamu jambo hilo?

242 Lakini, kumbukeni, Kanisa liliingia, pia, wale wafia imani wa Kanisa, walikuwa kwa ajili ya Neno la Mungu na ushuhuda wa Yesu Kristo. Ni wangapi wanaojua jambo hilo, hapa kwenye ninii . . . [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naam. Vema.

243 Sasa, lakini hawa hawakuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo.

. . . kwa ajili ya Neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao.

244 Wale Wayahudi! Na Hitler aliwachukia, vivyo hivyo na Eichmann, na Stalin pia, ulimwengu mzima uliosalia. Mnaona? Lakini wao walidumu waaminifu kwa yale waliyoamini. Nao waliwaua kwa sababu walikuwa ni Wayahudi.

245 Hivi mlifua ya kwamba Martin Luther kwa namna fulani alikuwa na wazo lilo hilo, pia? Ni kweli. Yeye alisema, "Wayahudi wote wanapaswa kuangamizwa. Wao ni wapinga-Kristo." Unaona? Lakini yeye alikuwa tu chini ya kipindi kingine cha wakati, wala hakuelewa na jambo hilo, hakulielewa Neno.

246 Sasa Neno, Kweli, inatokea. Utaendaje wakati wo wote kuwapofusha Israeli? Huwezi kufanya jambo hilo. La.

247 Loo! huyo nabii angewezaje kusimama pale, siku ile, na aseme, "Unaonekana kama nyati, ee Israeli?" wakati walipokuwa wakijaribu kumwonyesha sehemu zake zilizo mbaya kuliko zote! Yeye alisema, "Mbona," yeye alisema, "yeye akubarikiye atabarikiwa, na yeye akulaaniye atalaaniwa." Hiyo ni kweli. Loo, jamani! Utafanyaje jambo hilo?

248 Wakati mmoja wao walifikiri Mungu angesahau, wakati nabii alipoona kile kitu cheusi kikiwajia Wayahudi. Huyu mtu akiwa amesimama pale, Na Neno la Mungu likamjilia. Akasema, "Ee Bwana, utawaacha watu Wako?"

Yeye akasema, "Ni kitu gani hicho kilicho karibu nawe?"

Anasema, "Kijiti cha kupimia."

249 Kasema “Mbingu ina urefu gani? Ipime.” A-ha. “Bahari ina kina gani?”

Akasema, “Siwezi kuipima.”

250 Akasema, “Wala Mimi siwezi, wala Mimi siwezi sikuzote kuwasahau Israeli.” La, bwana. Yeye hatamsahau.

251 Ilimbidi kumpofusha mwanawe Mwenyewe. Sasa, wazia jambo hilo. Kumpofusha mwanawe Mwenyewe, apate kutupa sisi nafasi, nasi tunaikataa. Sasa, hilo halikufanyi ujisikie mdogo sana hata ungeweza kutambaa chini ya kipande kikubwa cha saruji huku umevaa kofia ya galoni ishirini, na hata usiliguse jambo hilo? Hilo ni dogo sana, unajua. Loo! jamani! Naam.

252 “Wao walilishikilia Neno la Mungu.” Walikuwa Wayahudi. Walikuwa na torati yao; walidumu nayo. Mnakumbuka jana usiku, sasa? Mnaona? Walidumu nayo. Nao walikuwa Wayahudi, nao walikuwa na torati. Na torati ilikuwa ni Neno la Mungu, nao walidumu nayo kwa uaminifu. Hiyo ni kweli. “Na kwa ushuhuda waliokuwa nao, walifia imani yao.” Na hapa zilikuwapo zile roho chini ya madhabahu, baada ya Kanisa kuondoka.

253 Sasa angalia. Wao walikuwa, katika upofu wao, wamemwua Masihi wao, na sasa wao walikuwa wakijutia jambo hilo. Walifahamu hilo. Walilitambua, baada ya kupita. Walimwona wakati huo, walipokuja mbele ya madhabahu ya Mungu. Lakini sasa neema ya Mungu iko juu yao.

254 Angalieni. Sasa, wao wasingeweza, kwa namna yo yote, kuwa ni watakatifu, maana wao tayari wamepewa nguo ndefu. Lakini hawa hapa sasa, ni “roho chini ya madhabahu, kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda waliokuwa nao” tu, kwamba wao ni watu wa Mungu, Wayahudi.

255 Lakini sasa, angalieni, neema ya Mungu inawajilia. Na Yesu anawapa, kila mmoja wao, nguo ndefu nyeupe, (loo! jamani! angalia; moja kwa moja huko ng’ambo, baada ya Kanisa kuondoka), kwa sababu walikuwa waaminifu kwa msimamo wao. Nao walipofushwa, wala hawakujua jambo hilo. Hawakulijua. Walikuwa wakitekeleza kikamilifu sehemu ile ambayo Mungu alikuwa amewakusudia kuitekeleza. Na hapa, hapa, Yohana anaangalia kule ng’ambo na kuona roho chini ya madhabahu. Sasa angalia, yeye anazona hizo roho. Angalia vile anavyoziita.

Zinalia, “Bwana, hata lini?”

Angalia, “Muda kidogo tu zaidi.” Unaona?

256 Hebu tupate jambo hilo, tunapoendelea mbele, kupitia moja kwa moja katika Maandiko sasa. Wao wanafahamu walikuwa wamemwua Masihi wao. Unaona? Wala hawakujua jambo hilo, lakini baadaye walitambua. Wao waka—wao wakauawa, vivyo hivyo, kulipia jambo hilo hapo, kwa kutenda mabaya. Na sasa angalia ni jambo gani walilipaswa kufanya! Unaona, walikuwa

na hatia ya kuua, kwa hiyo wakauawa. Mnaona? Walipiga makelele, “Damu Yake na iwe juu yetu!” Mnaona? Hiyo ni kweli. Nao walipofushwa.

257 Sasa, kama wao hawangukuwa wamepofushwa; Mungu alisema. “Waacheni. Wao hawastahili.” Lakini kwa kuwa walipofushwa na Mungu, neema Yake iliwashukia. Amina! Nena kuhusu neema ya ajabu! Na kumpa kila mmoja wao nguo ndefu, kwa maana Israeli wote wataokoka, kila mmoja aliyeandikwa jina lake. Hiyo ni kweli. Yesu aliwapa nguo ndefu.

258 Kama vile Yusufu alivyowafanyia ndugu zake; ni kivuli. Angalia, wakati Yusufu aliposimama pale, na wakati yeye hatimaye... Yeye alijijulisha pale kwenye madhabahu, madhabahu yake mwenyewe, katika jumba lake la mfalme, kiti chake cha enzi. Yeye akasema, “Watu wote waondoke mbele zangu.” Mkewe alikuwa kwenye jumba la kifalme; mahali ambapo Bibi-arusi atakapokuwa.

259 Ndipo akawaambia, akasema, “Hivi ninyi hamnijui mimi?” Ala! anzungumza Kiebrania sasa. “Mimi ni ndugu yenu, Yusufu.” Loo! jamani!

Wakasema, “Basi, loo! utatupata.”

260 Kasema, “Hebu kidogo. Hebu kidogo. Mungu alifanya jambo hilo kwa kusudi fulani. Aliwafanya mnifukuze, kusudi apate kuokoa maisha.” Utukufu! Hilo hapo, kweli kabisa. Kasema, “Msininii, msijikasirikie.” Mnakumbuka Yusufu alisema hivyo? Alisema, “Msijikasirikie. Kila kitu ni shwari sasa. Yote yamekwisha. Mungu alinituma hapa, niwatangulie.”

261 Mnajua, Biblia ilisema watamwambia, watakapomwona amekuja, ilisema, “Tunaelewa, Wewe ni Masihi, tunajua. Lakini, lakini, na hayo makovu ni ya nini?” Unaona?

262 Yeye alisema, “Loo! niliyapata katika nyumba ya rafiki Zangu.” Ati marafiki?

263 Na ndipo watakapotambua jambo hilo, hao waliosalia, wale mia na arobaini na nne elfu, Biblia ilisema ya kwamba watajitenga, nyumba kwa nyumba. Na kuchukua siku nyingi, wakilia tu, na kuomboleza, na kutembea huku na huku ardhini; wakisema, “Tulifanyaje jambo hilo? Tulilifanyaje jambo hilo? Ni ajabu, tulimsulubisha Masihi wetu wenyewe.” Ilisema, wakilia kama vile jamaa waombolezavyo kwa ajili ya mwana wao wa pekee, “Tulilifanyaje jambo hilo?”

264 Hao Wayahudi, wao—wao ndio watu wa dini sana kuliko wengine wote ulimwenguni; waliochaguliwa na Mungu. Lakini Yeye aliwapofusha, apate kutuchukua, nasi tunamkataa. Ni hukumu ya jinsi gani kwa kanisa la Mataifa! Hilo hapo. Unaona? Wamepofushwa makusudi, na Mungu, ili kwamba Yeye aweze kutupata, Bibi-arusi kwa ajili ya Yesu. Akawatoa katika...

Unaona? Na ilionyeshwa katika mfano kivuli huko nyuma, na kila kitu.

²⁶⁵ Sasa mnaona hizo roho ni akina nani? Hao si watakatifu waliokufa kishahidi. Watakatifu tayari wameshaondoka. Hiyo ni kweli. Angalia, hao walikuwa, hao walikuwa wameondoka tayari. Mnaona?

²⁶⁶ Kwa hiyo, hawa wanapewa nguo ndefu, kila mmoja wao. Na sasa nawatakeni mwone. Lakini sasa neema ya Mungu inawashukia. Yesu anawapa kila mmoja wao nguo ndefu nyeupe, kama Yusufu alivyofanya, neema yake kwa ndugu zake.

²⁶⁷ Sasa angalia. Ingawa walikuwa wamejaribu kumwua Yusufu, pia, lakini neema yake iliwashukia moja kwa moja. Unaona? “Loo! ni sawa. Hiyo ni sawa. Hamkumaanisha kufanya jambo hilo. Lakini, mnaona, hiyo ilikuwa ni Mungu akifanya jambo hilo. Unaona? Mungu aliwaruhusu ninyi nyote kufanya jambo hilo ili aweze kunifukuza, na kunileta huku ili kwamba niweze kuyahifadhi maisha ya watu, hawa Mataifa hapa, mahali nilikomtoa mke wangu. Singeweza kuwa na mke kama—kama ningalibaki kule nyumbani. Sasa, nampenda mke wangu. Amenizalia watoto hawa hapa.” Kisha kasema, “Mimi—mimi. . . Na sasa—sasa ninakuja kuwachukueni ninyi nyote. Sasa nyote mtakuwa na wakati mzuri kweli, pia. Nitawaleta huku. Sote tutaishi pamoja, kama jamaa moja kubwa.” Unaona? Unaona? Unaona? Kasema, “Ninataka kuwaulizeni jambo moja. Je! Baba yangu mzee angali anaishi? Loo!

²⁶⁸ Basi mwangalie, alichomfanyia mtoto Benyamini, ambaye ni mfano wa wale mia na arobaini na nne elfu, kama tutakavyoona baadaye. Mnaona alilofanya? Yeye alimkimbilia tu Benyamini moja kwa moja, akamwangukia shingoni na kuanza kumkumbatia. Ndugu yake mdogo aliyekuwa amezaliwa katika jamaa yake baada ya yeye kuondoka, unaona; na mama yake, lile kanisa la kwanza, kanisa la Kiorthodoksi. Wale mia na arobaini na nne elfu walizaliwa akiwa hayuko, wakati Yeye alipokuwa ameondoka kwenda kumtafuta Bibi-arusi Wake Mmataifa. Loo! jamani! Hilo haliwafanyii jambo fulani! Hilo hapo. Kwa hiyo mnaona hao ni akina nani? Hao hapo.

²⁶⁹ Angalieni sasa, ingawa walikuwa wamejaribu kumwanganiza Yusufu, neema yake iliwafikia.

²⁷⁰ Ingawa walikuwa wamejaribu kumwanganiza Yesu, Yeye angali anarudi moja kwa moja (maana wao walikuwa vipofu) na kuwapa, kila mmoja wao, nguo ndefu nyeupe. Yeye atawapeleka awaingize moja kwa moja, nyumbani, hata hivyo. Haileti tofauti yo yote, maana Yeye tayari amesema, “Nitawaokoa wote, hata hivyo.” Mnaona?

Sasa kifungu cha 10. Angalieni, wao waliomba “wapatiwe haki.” Unaona?

271 Sasa, kama ingekuwa ni Bibi-arusi, ingalikuwa kama kile cha Stefano. “Baba, wasamehe,” unajua. Unaona?

272 Lakini hawa ni Wayahudi ambao ndio kwanza waingie, unaona. Wao waliomba “wapatiwe haki.” Angalieni tena, mnaona, Yeye alisema tena. . . Angalieni, si. . . Yeye alisema, “Ni ndugu zako,” wale Wayahudi. Wale mia. . . Sasa wao walitaka kulipiza kisasi. Walisema, “Loo! tutaniii. . . Sisi, tunataka Wewe utulipizie kisasi kule chini.”

273 Akasema, “Kitambo kidogo tu, sasa, muda kidogo tu.” Kwa maana, angalia, hebu nilisome hapa. Liko kwenye—kwenye aya ya 10. Vema.

Nao wakalia kwa sauti kuu, wakisema, Ee Mola, Mtakatifu, Mwenye kweli, hata lini kutokuhukumu, wala kuipatia haki damu yetu kwa wao wakaao juu ya nchi?

Nao wakapewa kila mmoja nguo ndefu, nyeupe, wakaambiwa wastarehe bado muda mchache, unaona, (ati nini?) muda mchache, hata wajoli wao. . .

274 Mnaona? Sasa ni kitu gani? Wale manabii sasa wanawahubiria Israeli. Mnaona?

. . . hata itakapotimia hesabu ya. . . wajoli wako pia. . . wajoli wako na pia ndugu zako, watakaouawa. . .

275 Unaona? wale waliochaguliwa tangu zamani kufanywa hivyo. Mnaona?

. . . watakaouawa vile vile kama wao itakapotimia

276 Mnaona, kwa maneno mengine, wamechaguliwa tangu zamani. Ni Maandiko, ya kwamba hawana budi kufanya hivyo. “Na wapumzike tu muda kidogo. Sasa mmepata nguo zenu ndefu; mnaenda nyumbani; basi kaeni tu hapa kidogo, mnaona, ngojeni kidogo tu.”

277 Sasa angalia. Sasa angalia, “Ndugu zako.” “Hao ndugu zako ilibidi kwanza wauawe,” ambalo linamaanisha wale mia na arobaini na nne elfu ambao wangali wataitwa wakati wa ile Dhiki. Wale mia na arobaini na nne elfu ambao wanaitwa.

278 Laiti tungalikuwa na wakati. Huenda tukaupata kesho usiku, Bwana akipenda, sisi. . . kabla tu hatujaingia kwenye ule Muhuri mwingine. Unaona?

279 Pia, sasa angalieni, hao hawana budi kuuawa kwa ajili ya imani yao na mpinga-Kristo. Tumeyapitia hayo sasa hivi tu; basi angalia, katika kule kupanda farasi kwake kwa mwisho, ambapo yeye anavunja—anavunja agano hilo na hao Wayahudi kule. Na huyo hapo anaenda. Unaona?

280 Wayahudi hawa, wale mia na arobaini na nne elfu, wataitwa na wale mashahidi wawili wa Ufunuo 11. Sasa, mnakumbuka, walikuwa watoe unabii.

281 Mmesoma jambo hilo. Ni wangapi wamesoma jambo hilo? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Hakika, sote tunajua, kwa kusoma Maandiko.

282 Nao wanatoa unabii, hawa mashahidi wawili wanatabiri, katika wakati wa nusu ya pili ya juma la sabini la Danieli. Hiyo ni ile miaka mitatu na nusu ya mwisho.

283 Mnakumbuka jinsi tulivyoyachukua yale majuma sabini ya Danieli? Nilisema tutayahitaji tutakapofikia hapa. Sikujua ni kwa nini, lakini mimi nilininii tu. . . Kitu fulani kiliniambia ya kwamba tungeyahitaji, nasi tumepafikia. Naam. Unaona?

284 Angalia, katika wakati wa Danieli. Sasa kumbukeni, Danieli aliambiwa ya kwamba, "Masihi angekuja," yule mtawala, "Masihi," hasa, "naye angetabiri. Israeli bado walikuwa na majuma sabini yaliyosalia. Na katikati ya yale majuma sabini, Masihi atakatiliwa mbali, na ile dhabihu ya kila siku itaondolewa." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Lakini bado kulikuwa na majuma matatu na nusu, yaliyokusudiwa."

Katika kipindi hiki, Yeye anachukua Bibi—arusi Mmataifa.

285 Sasa, Yeye anapaa juu. Na wakati atakapopaa juu, manabii wawili wanainuka kwa ajili ya Israeli. Mnaona?

286 Na roho hizo ambazo zimekwisha uawa kishahidi, sasa, katika zamani zote hizi hapa, Wayahudi halisi na wa kweli, tokea zamani huko; waliokuwa wameandikwa majina yao katika kile Kitabu, ambao waliishi maisha mazuri na kutenda haki, walioishi kiaminifu kabisa katika dini ya Kiyahudi. Wao, wao waliuawa na Eichmann na wengine wengi. Watu wanyofu wa moyo, mamilioni yao zamani huko! Na hao Wajerumani waliwapiga risasi wakafa, na wakawaua maksudi, na wakawaua, na kuwanyonga juu ya fensi, na kuwachoma moto, na kuchoma maiti zao, na cho chote kile. Huyu Hitler asiye na damu, ama mwenye kupenda kumwaga damu, mwenye njaa ya damu, na Stalin, na Mussolini, na hao watu wote waliowachukia hao Wayahudi!

287 Nafikiri hilo ndilo moja ya—moja ya mambo ambayo yanalishikilia taifa hili pamoja, maana wao daima wamewaheshimu Wayahudi, hiyo ni kweli, wakampa makao. Ukimheshimu Myahudi, basi Mungu atakuheshimu.

288 Sasa, kuna kundi la Wayahudi ambao ni wahuni, kama tu vile vile kulivyo na Mmataifa.

289 Lakini Myahudi halisi, Mungu ameliandika jina lake kwenye kile Kitabu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Naye huyu hapa, ameuawa katika wakati huu. Pia kumbukeni, hebu

wazieni jambo hilo sasa, vile jambo hili lilivyo sahihi. Mara baada ya hao mamilionni ya Wayahudi kuuawa, watu wasio na hatia, na mataifa ya dunia; hapa Maandiko yanasema, katika wakati huu huu, ya kwamba kila mmoja wao yuko chini ya madhabahu, wanatambua kile kilichotukia, nao wanapewa nguo ndefu nyeupe.

290 Nao wakasema, “Vema, kwa nini? Tunaweza kurudi kwenye ufalme sasa hivi?” Ufalme wa Wayahudi utanzishwa duniani, mnajua. Yohana alisema ufalme ulikuwapo, mnaona, utanzishwa.

Sasa, huu ni Ufalme wa Injili, unaona.

291 Lakini ufalme wa Wayahudi utahubiriwa na hawa—hawa manabii wawili, kwa hiyo angalia u—u—ufalme wa hapa duniani.

292 “Ufalme wa Mbinguni unahubiriwa,” . . . na Wayahudi, ama kwa . . . ninamaanisha, “kwa Mmataifa.”

293 Ufalme wa hapa duniani, utanzishwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu, baada ya, ule Utawala wa Miaka Elfu kwa Wayahudi.

294 Sasa angalia. Angalia jambo hili sasa, hapa, wakati wao—wakati wao wanahubiri, unaona.

295 Kabla ya hawa—hawa manabii kuja jukwaani; hawa Wayahudi waliopaswa kufa chini ya Eichmann na hao wengine, kila mmoja wao aliyechaguliwa tangu zamani, anapewa (kwa neema) nguo ndefu nyeupe. Kila mmoja wao anapewa nguo ndefu nyeupe. Angalia.

Sasa ni jambo gani linalotukia? Mara jambo hilo linapotukia . . .

296 Ninaangalia ile saa kule nyuma, nami najua tuna—tunachelewa. Lakini sitaki ku- . . . unaona, ni—ni . . . Hao . . . ninawaangalia maskini watu hao wamesimama pale. Mungu awasaidie, ndugu. Natamani kila mmoja wenu apewe nguo ndefu nyeupe kwenye siku ile, unaona. Huku mmesimama, mkibadilishana huku na huko, huku miguu inauma. Na baadhi yenu mlifanya kazi siku nzima. Ninajua ni kitu gani mnachokipitia. Na angalieni hapa . . . Na baadhi ya maskini wanawake wazee wamesimama. Nimeona baadhi ya hawa wanaume wakiwapa wanawake viti vyao; na mtu mwingine amempisha, maskini mwanamke mmoja kijana aliye na mtoto mchanga. Nami ni—ni—ni—ninaona hayo yote, mnaona, nami nina hakika Yeye anaona. Angalieni. Lakini sitaki kuwaweka kwa muda mrefu sana. Kama ningeweza tu kuwafanya mwone Ujumbe, ni hilo tu ninalowataka mwone, mnaona.

297 Sasa angalia Wayahudi hawa. Sina budi kufanya jambo hili, kusudi niwaonyeshe ufunuo wa Muhuri huu; mwone ni kitu gani,

roho hizi chini ya madhahabu, na kwamba wao ni akina nani. Sasa angalieni.

²⁹⁸ Katika wakati wa Danieli, sasa, ile sehemu ya pili ya lile juma la sabini. Sasa kumbukeni, “Masihili alikuwa akatiliwe mbali katikati.” Yaani katikati. Vema, nusu ya saba ni nini? [Kusanyiko linasema, “Tatu na nusu.—Mh.] Tatu na nusu. Kristo alihubiri muda gani? [“Mitatu na nusu.”] Hilo ni sawa. Sasa, “Lakini kumekusudiwa bado, kwa watu,” (kitu gani?) “miaka mingine mitatu na nusu.”

²⁹⁹ Vema, katika kipindi cha wakati huu, mbona, unaona, yale yanayotukia, ni kwamba, Bibi-arusi Mmataifa anachaguliwa katika nyakati saba za kanisa, na anapaa juu.

³⁰⁰ Na wakati hilo linapotendeka, Wayahudi hawa wote ambao waliuawa kwa ajili ya imani yao kule kwa sababu ya upofu, wakiwa wamepuzika chini ya mdhabahu, Mungu anakuja na kusema, “Mnaona ilikuwa ni kitu gani? Sasa nampa kila mmoja wenu nguo ndefu nyeupe.”

Wakasema, “Hata lini, Bwana? Je! Tunaingia sasa?”

³⁰¹ Kasema, “La, la, la, la. Wajoli wenu, Wayahudi, hawana budi kuteseka kidogo, bado. Hawana budi kuuawa kama mlivyouawa. Yule mnyama hana budi kuwatesa wakati atakapovunja agano lake.”

³⁰² Sasa angalia. Na sasa angalia, mara tu... Sasa kumbuka tu, manabii hawa watatabiri kulingana na Ufunuo 11. Ninyi, mlioinua mikono yenu, mlikwisha kulisoma. Mnaona? Nao wanapewa uwezo.

³⁰³ Nasi tutaenda kuona hao ni akina nani, mnamo dakika moja tu, Bwana akipenda. Sasa, angalieni hawa manabii ni akina nani. Na sasa Biblia inaliongelea jambo hilo hapa. Hakika, Yeye analielezea. Hakika! Unaona?

³⁰⁴ Sasa, angalia, katikati ya haya majuma matatu na nusu sasa, ambayo wanatabiri hapa chini na U—Ufunuo hapa ilisema... Nao—wao walitabiri siku elfu moja na mia mbili na sitini. Kama... .

³⁰⁵ Sasa, kalenda ya kawaida ya Wayahudi, wakati wa kawaida wa kalenda ya Mungu, ni miezi thelathini kamili katika mwezi. Ie kalenda ya Kirumi, ndiyo iliyochanganya. Kalenda ya kawaida ni siku thelathini kwa mwezi.

³⁰⁶ Sasa, kama ukitaka kuchukua siku thelathini, na kuongeza miaka mitatu na nusu kwake, na kuona siku thelathini, na, vema, unapata nini? Elfu moja mia tatu na... ama mia mbili sitini. “Siku elfu moja mia mbili na sitini (siku sitini),” miaka mitatu na nusu kamili.

³⁰⁷ Sasa, unaona, hakuna kosa hapo. Hilo hapo, inalingana barabara kama ku—kuumanisha mbao pamoja. Angalia, hao manabii wawili walihubiri kwa miaka mitatu na nusu, kwa

Wayahudi. Katika wakati huo, wanaitwa watoke, wale mia na arobaini na nne elfu.

308 Na halafu, angalia, hawa manabii wawili ni Musa na Eliya wenyewe hasa. Unaona? Unaona? Sasa angalia, angalia, ninii yao. . . Angalia huduma yao. Sasa angalia yale manabii hawa wanayofanya. “Hao wana amri ya kuipiga nchi kwa pigo, kila watakapo.” Ni nani aliyefanya jambo hilo? Musa. “Wana amri ya kuzifunga mbingu, ili mvua isinyeshe katika siku ya unabii wao.” Ni nani aliyezifunga mbingu kwa muda wa miaka mitatu na nusu? [Kusanyiko linasema, “Eliya.”—Mh.] Hao hapo. Ndio hao. Unaona, ni . . .

309 Unaona, mtu, wakati anapokufa, yeye habadilishi hali yake. Yeye habadilishi tabia yake, unaona. Angalia, wakati— wakati, kabla . . .

310 Wakati Sauli alipokuwa amerudi nyuma, na hakukuwa na manabii nchini, hakuweza kufahamu la kufanya—la kufanya. Alikuwa anakabiliwa na mambo mazito sana. Alikuwa anaenda vitani. Alienda kwa yule mchawi wa Endori.

311 Sasa, ikiwa ni damu tu ya mafahali na mbuzi, yule mwanamke mchawi aliweza kufanya jambo hili. Ndipo akaita roho ya Samweli.

312 Na Samweli alipotokea, huyo hapo amesimama, katika joho lake la nabii. Isitoshe, lakini alikuwa angali ni nabii. Akasema, “Kwa nini uliniita kutoka kwenye mapumziko yangu,” unaona, akasema, “kwa kuwa wewe umekuwa adui wa Mungu?” Akasema, “Katika wakati huu, kesho usiku, utaanguka vitani. Na wakati huu, kesho usiku, utakuwa pamoja nami.” Na hilo ndilo lililotukia hasa. Unaona? Si ninii tu. . . Yeye alikuwa angali nabii. Mnaona?

313 Na jamaa hawa wangali ni manabii. Sasa tutaingia kwenye kilindi kidogo katika jambo hilo, mnamo dakika chache tu, Bwana akipenda. Unaona?

314 Loo! jamani! jinsi ninavyolipenda Neno hilo! Si ajabu, “Mtu hataishi kwa mkate tu. Kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu!”

315 Manabii hawa wawili ni Musa na Eliya, kulingana na kazi zao zinazofanana tena. Hiyo, hiyo daima imekuwa ndiyo huduma yao. Sasa angalieni, kama tu walivyofanya. Hilo halikuwabadilisha. Kumbukeni, jamaa hawa hawakufa kamwe. Angalia kwa dakika moja tu.

316 Sasa, usichanganye, kabla hatujaliacha jambo hili. Msichanganye huduma ya tano ya Eliya na huduma yake ya nne. Nimekuwa nikiwaambia, Kanisa la Mataifa linamtazia Eliya. Kweli.

317 Na ndiye huyu hapa upande huu pamoja na Wayahudi. Kumbukeni, yeye hawezi kuja mara nne; hiyo—hiyo ni namba ya adui. Hana budi kuja mara tano.

318 Alipokuja kwa mara ya kwanza, alikuwa ni Eliya, mwenyewe. Alipokuja mara ya pili, alikuwa ni Elisha. Alipokuja tena, alikuwa (nani?) Yohana Mbatizaji. Ajapo tena, ni kwa ajili ya malaika wa saba. Na anapokuja mara ya tano, yeye yuko pamoja na Musa upande ule, akiwahubiria. Hakika. Naam, bwana. Usimchanganye. A-ha.

319 Tano, kama unajua nambari za—zako za Biblia, tano ni namba ya neema itendayo kazi. Na hivyo ndivyo Yeye alivyofanya. Sasa, angalia, unataka kujua ni wapi. Je! Yesu alikuwa kazi ya neema? J-e-s-u-s (Yesu) tano, b-i-d-i-i. Hiyo ni kweli? Bidii, kwa ajili ya—kwa ajili ya kukupenda wewe. Na kama utafika Kwake, unakujaje, kwa njia gani? I-m-a-n-i katika kufanya bidii. Sivyo? Bidii ni namba ya neema, vema, kwa waamini.

320 Angalia, Eliya wa kwanza, huyo alikuwa ndiye. Wa pili alikuwa ni Elisha. Wa tatu alikuwa ni Yohana. Wa nne alikuwa ni yule malaika wa saba, ama yule mjumbe wa mwisho kwa Kanisa, kulingana na Malaki 4 na Ufunuo 10:7. Sasa, mara ya tano, yeye ni mjumbe kwa Wayahudi, kwa wale mia moja na arobaini na nne elfu, kwa Wayahudi, baada ya Kanisa kuondoka.

321 Ni—ni—ninajisikia wa ajabu-ajabu tu kidogo, unaona. Unaona? Angalia, kama wengine wanafikiri. . . Ninawataka mwelewe na jambo hili sasa, mnaona. Kama wengine wangali wanafikiri ya kwamba Malaki 4, “kuwarejesha” watu, ni jambo lile lile atakalofanya kule kwa Wayahudi, na anafikiri yote ni mambo, hebu nilinyoshe jambo hilo kwa ajili yenu, dakika moja tu. Unaona, lingekuwa jambo la kutatanisha kidogo. Maana, kumbukeni, katika Malaki 4, inasema, “Kuigeuza Imani ya baba zao. . . ama watoto iwaelekee baba zao.” Mnaona, kuwarudia baba zao!

322 Sasa hebu niwaonyeshe tofauti za huduma hiyo. Kama akija kuigeuza Imani ya watoto iwaelekee baba zao, yeye angemkana Kristo. Angerudi kwenye torati. Hiyo ni kweli? Baba walishika torati. Mnafahamu jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

323 Angalia, wakati Elisha, wakati alipokuja kuitimiza huduma yake katika Malaki 4, unaona, kama Malaki 4, Eliya alikuwa peke yake.

324 Lakini anapokuja kuwahudumia Wayahudi, wa Ufunuo 11, ameambatana na Musa. [Ndugu Branham anapiga makofi mara mbili—Mh.] Kwa hiyo, hakuna utata, hata kidogo. Unaona? Mnaelewa jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”]

325 Wakati Elisha anapokuja, wa Malaki 4, yuko peke yake. Eliya atatekeleza; si Eliya na Musa. “Eliya” atatokea. Lakini

upako ule ule, ambao, ulisema Eliya atakuja kwa ajili ya sehemu ya mwisho ya wakati wa kanisa, “kuigeuza Imani ya watoto ielekee kwenye Imani asili ya baba zao,” Imani ya mitume, ambayo mnapaswa kuirudia. Na mpinga-Kristo amewavuta akawatoa wote nje. “Kuigeuza,” kama vile Maandiko mengine yote yalivyopatana. Unaona, yeye anakuja peke yake. Unaona?

³²⁶ Lakini atakapokuja kwa Kanisa, Biblia . . . ama atakapokuja kwa wale mia na arobaini na nne elfu, Biblia inasema dhahiri ya kwamba yeye pamoja na . . . Wako wawili, si mmoja wao. Wawili! Na huduma yake ya kwanza haingeweza kuwachukua Wayahudi na kuwarudisha kwenye torati, kwa sababu yeye . . . maana yeye anakuja, akimhubiri Kristo kwa wale mia na arobaini na nne elfu, amina, “Huyo hapo, yule Masihi aliyekatiliwa mbali.” Amina! Hivyo ndivyo ilivyo, kwa hiyo usilichanganye. Si la utata. Maandiko hayasemi uongo, hata kidogo.

³²⁷ Utukufu! Loo! nilipoona jambo hilo, nilikuwa nikiruka! Nikasema, “Asante, Bwana,” nilipokuwa nikiangalia jambo hilo likitukia pale. Nilimwona Eliya akienda zake pale kwa ajili ya ule wakati wa kwanza, akiwa peke yake, naye alikuwa peke yake. Halafu nilipomwona akija tena, huko mbali akielekea mahali pengine, walikuwa ni wawili pale wakati jambo hilo lilipotukia. Kasema, “Hilo hapo. Hilo, hilo latosha, Bwana. Amina! Ninaliona sasa! Haleluya!” Hilo ni kweli kabisa.

³²⁸ Kama sikuwa nimelitaja, lingekuwa kidogo linamtatiza mtu. Lakini Yeye—Yeye aliniambia niseme jambo hilo, kwa hiyo nimelisema.

³²⁹ Angalia, watu hawa wamehifadhiwa hai na Mungu, toka katika huduma yao ya kwanza, kwa ajili ya huduma ya siku za usoni; waliitumikia vizuri sana. Unaona? Wazienu tu, roho hiyo ya Eliya inahudumu mara tano; Musa, mara mbili. Ati nini? Wamewekwa hai kwa ajili ya huduma yao ijayo, huduma ijayo.

³³⁰ Wala hakuna mmoja wa hao wawili aliyekufa sasa; msiamini jambo hilo. Wote wawili walionekana, wakiwa hai, wakizungumza na Yesu kwenye Mlima wa Kugeuzwa Sura. Lakini, kumbukeni, wao hawana budi kufa.

³³¹ Lakini, sasa, Musa kweli alikufa. Bali alifufuka, maana Yeye alikuwa ni mfano mkamilifu wa Kristo. Mnaona? Hakuna mtu amepata kujua mahali alipozikwa. Malaika walikuja wakamchukua. Mnaona? Jeneza lake lilibebwa na Malaika. A-ha. Kwa nini? Hakuna binadamu angaliweza kumbeba kumpeleka alikokuwa akienda. Yeye alipitia katika tendo fulani fulani, basi. Waliobeba jeneza lake, walikuwa ni Malaika, unaona, maana Wao walimchukua wakampeleka alikopaswa kuwa. Hakuna mtu ajuaye.

³³² Hata Shetani, hata hakujua. Alishindana na Malaika Mkuu. Hiyo ni kweli. Hakuelewa yaliyompata Musa. “Nilimwona akitetemeka kule. Na akiangalia ile nchi, kisha akigeuka na

kuwaangalia wale wana, na kadhalika, nilimwona akitetemeka. Lakini alikanyaga juu ya ule Mwamba, na hiyo ilikuwa ndiyo mara ya mwisho niliyomwona.”

333 Huo ndio ule Mwamba! Huo ndio ule Mwamba! Naomba nisimame kwenye Mwamba huo, mwisho wa safari yangu! Ndio, bwana! Sasa, wale. . . Ndugu zangu weusi walikuwa wakija hapa na kuimba wimbo mfupi, “Kama ningaliweza, hakika ningesimama kwenye ule Mwamba ambapo Musa alisimama.” Ndio, bwana! Loo! huo ndio Mwamba ule ninaotaka kusimama juu yake, pia. Kwa imani ninasimama pale.

334 Lakini kumbuka, Eliya, yeye alichoka tu, maana alikuwa na kazi nyingi sana mbele yake. [Ndugu Branham anatulia. Kusanyiko linacheka—Mh.] Kwa hiyo alikuwa amechoka sana, ndipo Mungu akamtumia gari la kumpeleka Nyumbani, hiyo ni kweli, akatuma gari. Hiyo ni kweli? [“Amina.”] Likampandisha juu. Yeye hakufa hata kidogo, maana Yeye alimweka hai. Yeye alikuwa na kazi ya siku zijazo kwa ajili yake. Akamwacha amtie mafuta mtu fulani, pia, unaona, akatokea katika Roho yake.

335 Lakini hawana budi kuonja mauti. Sasa Ufunuo, mlango wa 11. Sasa, hebu twende, ninaenda moja kwa moja hapa hata hivyo. Hebu na tufungue tu, Ufunuo 11. Angalia uone kama hao wawili hawauawi. Naam, bwana. Wote wawili hawana budi kuonja mauti. Naam, bwana. Baada ya huduma yao kwisha, wanaonja mauti. Ufunuo 11, na tuanzia ya 7.

Na hata wa- . . . watakapoumaliza ushuhuda wao, yule mnyama atokaye katika kuzimu atafanya vita nao, . . .

336 Loo! jamani, yeye hawezi kuvumilia jambo hilo; hao watakatifu wanaojivingirisha wamerudi tena, unaona. Vema. Vema.

. . . atokaye katika kuzimu . . . anafanya vita nao, naye atawashinda na kuwaua.

337 Lakini angalia jambo linalotukia. Wao wameonyeshwa kwa mfano kikamilifu sasa.

Na mizoga yao itakuwa katika njia—katika njia ya mji ule mkuu, uitwao kwa jinsi ya roho Sodoma, na Misri, tena ni hapo Bwana wetu aliposulubiwa. (Yerusalemu, unaona.)

338 Sasa hawana budi kuonja mauti, (sivyo?) hiyo ni kweli, baada ya huduma yao kwisha.

339 Kwa Nini? Huduma ya malaika wa saba, huduma ya malaika wa saba, huduma ya Eliya kwa malaika wa saba, si. . . Mbona, kwa nini haingeweza, hasa, ninajaribu kusema, huduma ya malaika wa saba basi iwe ni ya Musa, kama yeye hajafa, jinsi vile vile tu ambayo ingalikuwa ya Eliya? Mbona wao hawaninii. . . Kwa nini Mungu hakumtuma tu, aseme, “Eliya, wewe—wewe

umefanya kazi kwa bidii sana, mimi . . . na kila kitu, mahali hapa pote mbalimbali. Na—nadhani nitamtuma tu Musa”? Kwa nini?

³⁴⁰ Angalia huduma ya Musa. Eliya alikuwa nabii kwa mataifa yote, lakini Musa alikuwa mtoa sheria kwa Wayahudi peke yao. Amina. Musa yuko pale kusema . . . Sababu ya yeye kuambatana na Eliya . . . Hao Wayahudi wakisema, “Ngojeni, tungali tunashika torati hapa.” Lakini huyu hapa amesimama Musa mwenyewe; na huyu hapa Eliya amesimama pamoja naye. Loo! Unaona? Yeye anakuja kwa ajili ya Wayahudi peke yao. Unaona? Musa aliwaendea Wayahudi peke yao; nabii Eliya alikuwa kwa ajili ya mataifa yote. Lakini Musa alikuwa nabii kwa ajili ya Wayahudi, na mtoa sheria. Unaona? Huo ndio uliokuwa ujumbe wake, ile sheria.

³⁴¹ Lakini ujumbe wa Eliya ulikuwa ni nini? Kwa wanawake waliokata nywele zao; madhehebu. Naam, bwana. Naye kweli aliwararua vipande-vipande. Nyuso zilizopodolewa; akawaambia, “Mtalishwa kwa mbwa.” Yeye aliwakemea tu kwelikweli.

³⁴² Na halafu wakati Roho yake ilipomjilia Yohana, yeye alitokea haraka kutoka nyikani na kufanya jambo lile lile. Kweli. Akasema, “Msifikiri ya kwamba sisi ni wafuasi wa *hiki* ama *kile*. Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.”

³⁴³ Akapandisha zake barabarani, akasema, “Na unataka kuniambia ya kwamba ulimwoa nanii wa shemejio yako mwenyewe . . .?” Akasema, “Si halali kwako kufanya hivyo!” Loo! ndugu! Whiu! A-ha! Alimkemea kweli kweli. Hakika.

³⁴⁴ Angalia, roho hizi hazina budi kungojea kitambo kidogo, kwa ajili ya wale mia na arobaini na nne . . . watakaouawa kwa ajili ya imani yao. Loo! si hilo, je! hilo si ninii . . . Hilo linaiunganisha tu Biblia pamoja.

³⁴⁵ Sasa wakati wangu umekwisha kabisa, kama nikiwaachilia mapema. Lakini nina mambo mengine machache zaidi kidogo tu ya kusema, kama mnaweza kuyavumilia. [Kusanyiko linasema, “Endelea!”—Mh.] Ninajua kuna joto. Nami ninatoka jasho.

³⁴⁶ Lakini, sikilizeni, nina jambo fulani tu la kuwaambia. Ni zuri sana, linanichoma tu ndani kabisa moyoni mwangu. Ninatumaini hamjalisahau, mnaona. Hebu niseme jambo hili, mbele Zake. Kwa neema Yake, Yeye aliniruhusu pia kuwaona watu wangu, si muda mrefu uliopita, wakiwa katika mavazi meupe. Mnakumbuka jambo hilo? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Mnakumbuka? Je! mnakumbuka hadithi hiyo, si muda mrefu uliopita? [“Amina.”] Bibi-arusi Mmataifa, wao wako kule hivi sasa. Wote walikuwa wamevaa nguo ndefu nyeupe.

³⁴⁷ Nilikuwa nimeamka. Nilikuwa nimetoka kwenye mkutano. Ilikuwa kama mwaka mmoja uliopita, zaidi kidogo. Niliamka asubuhi moja, na nikainuka. Kisha nikasema, “Mpenzi?”

nikimwambia mke wangu. Yeye hakushtuka. Wototo karibu. . . Ilinibidi kuamka na kuwapeleka shuleni, papa hapa juu kwenye ile nyumba ya zamani. Vema, ni—niliinuka kitandani, unajua, na kuegemea. Mnajua vipi; unaamka na kuketi tu na kuegemeza tu kichwa chako kwenye ubao wa kichwa cha kitanda. Tuna kimoja cha vile vitanda vya mtindo wa kizamani. Na kwa hiyo nilijiegemeza nyuma tu namna *hiyo*.

³⁴⁸ Ndipo nikawaza, “Aisee, wewe tayari una miaka hamsini na mitatu. Kama utamfanyia Mungu kazi yo yote, afadhali uanze kuifanya, maana utazeeeka sa—sana, baada ya kitambo kidogo.”

³⁴⁹ Ndipo nikawaza, “Unajua, hiyo ni kweli, sasa.” Nikawaza, “Aisee, unajua, mimi siko mbali sana. Sina budi kuondoka hivi karibuni sana.” Nikasema, “Huo, huo ni mwaka mmoja zaidi ya alivyoishi baba yangu.” Unaona? Nikawaza, “Sina budi kuondoka niende zangu hivi karibuni sana. Niliona jambo hilo. Na, hapa, sijamfanyia Mungu lo lote, bado.” Nikawaza, “Daima nilitaka kumfanyia Yeye jambo fulani.” Nikawaza, “Sina budi kuharakisha na kufanya jambo hilo, kama nitalifanya. Nami sijui nitakavyolifanya jambo hilo, ni hivyo tu.”

³⁵⁰ Nikawaza, “Jamani, ninatumaini kuishi nipate kuona kuja Kwake. Sitaki kuwa mzuka ama roho.”

³⁵¹ Unaona, daima nimekuwa nikiogopa roho. Na sasa, unajua, namna hiyo ya. . . daima nilifikiria, kama vile kwamba ningekutana na Ndugu Neville naye angekuwa wingu dogo jeupe likizunguka, unajua. Nami ningesema, “Aloo, Ndugu Neville.” Naye angesema, “Aloo, Ndugu Branham,” kwa hisi fulani nyingine; hangeweza kuongea. Lakini ningejua tu kwamba ilikuwa ni Ndugu Neville. Naam. Ningetaka kumpa mkono kama ninavyofanya sikuzote. Maana, hayo ndiyo tu nijuayo, ni wanadamu. Unaona, ningetaka kumpa mkono, lakini hana mkono. Uko kule chini kaburini, umeoza. Unaona?

³⁵² Nikawaza, “Jamani, natumaini haitanibidi kupitia kwenye jambo hilo.” Sasa, nilikuwa. . . Sasa nitawaambia kweli. Ni—nililogopa kufa; si kuogopa kwamba ningepotea, lakini sikutaka kuwa roho. Nilitaka kubaki mwanadamu. Nilitaka kungojea Unyakuo, unaona. Nilitaka tu kubaki namna hiyo. Sikutaka kuwa roho yo yote, kuzunguka-zunguka. Nilikuwa nimelala pale, nikiwazia jambo hilo.

³⁵³ Na, mara, kulikuwa na jambo fulani lililokatukia. [Ndugu Branham anadata kidole mara moja—Mh.]

³⁵⁴ Sasa, mnajua, na nyote mnafahamu sana, kuhusu yale maono. Na kama hili lilikuwa ni ono, sijapata kuona moja kama hilo, mnaona. Nami nimepata tangu nilipokuwa mvulana mdogo.

³⁵⁵ Ndipo, mara, jambo fulani likatukia. Nami nikajisikia nikiondoka. Nikawaza, “Aloo.” Nami ni—nikawaza, “Ni—

nimekufa tayari, unaona, na nime—nimekwisha ondoka.” Mnaona?

356 Nami nikafikia mahali fulani, na nikawaza, “Nadhani nitaangalia nyuma.” Ilikuwa ni dhahiri sana, enyi wapendwa, kama mimi ninavyosimama hapa sasa hivi. Unaona? Ndipo nikageuka, kuangalia nyuma. Nami nilikuwa niko, nimelala kitandani. Nami nilikuwa nimejinyosha, nimelala kando ya mke wangu.

357 Nikawaza, “Vema, labda ulikuwa ni ugonjwa mbaya wa moyo.” Unaona? Nikawaza, “Vema, unaona, nilikufa tu mara moja,” ambayo ingekuwa ni njia nzuri ya kuaga dunia. Kwa hiyo, nikawaza, “Huo ni ugonjwa mbaya wa moyo. Haikunibidi kuteseka.” Nikaangalia, nami nikawaza, “Vema, sasa, hilo ni jambo la kushangaza. Mimi niko pale nimelala, pale pale; na mimi hapa nimesimama, hapa.”

358 Kwa hiyo, nikageuka. Ilionekana kama—kama uwanja mkubwa sana, vile, ama cho chote kile, uwanja mkubwa sana tu ulioenea wa nyasi za buluu. Na—nami nikasema, “Vema, sijui hii ni nini?”

359 Na, mara moja, nilipokuwa ninaangalia, hawa hapa wanakuja maelfu mara elfu ya wanawake wasichana, wote wamevaa mavazi meupe, nywele zikining’inia mpaka kwenye viuno vyao, hawakuvaa viatu, nao walikuwa wananikimbilia moja kwa moja. Nikawaza, “Sasa hii ni nini?”

360 Nikageuka, nikaangalia *kule* nyuma, nami nilikuwa nipo pale; kisha nikaangalia juu *hivi*, hao wanakuja. Nikauma kidole changu. “Mi—mi—mi—mimi sijalala, kweli.” Lakini, niliweza kuhisi. Ndipo nikasema, “Vema, basi, jambo fulani hapa, ajabu hii.”

361 Na hawa wanawake wote wanakuja, mbio. Nami sijapata kuona wanawake wenye sura nzuri namna hiyo! Nao wote wakaja, wakinikimbilia. Nao waliponikimbilia. . .

362 Mnajua jinsi nilivyokuwa, kwa namna fulani. . . Wao huniita mimi mchukia wanawake, lakini mimi si mchukia wanawake, unaona. Lakini, na—nafikiri tu, mwanamke mwema ni mmoja wa . . . ni lulu. Lakini, nadhani, yule asiyefaa, ni, kama asemavyo Sulemani, “maji katika damu yako.” Kwa hiyo kwa kweli sina haja na—na mwanamke mwenye sifa mbaya ama wenye majivuno sana.

363 Na kwa hiyo wanawake hawa wote wakaja. Wakaanza kunikumbatia. Sasa, hilo si jambo la kawaida. Mnajua nisingevumilia jambo hilo. Kwa hiyo, nao walikuwa. . . Sasa, itanibidi kusema jambo hili kwa njia fulani, ya kwamba, ni—nina umati mchanganyiko. Lakini, wao walikuwa, walikuwa ni wanawake. Walikuwa wanawake. Nao—nao walinikumbatia, kila mmoja, na kusema, “Ndugu ye—yetu mpendwa!” Na mmoja angenikumbatia, na halafu huyo mwingine angenikumbatia.

364 Nilikuwa nimesimama pale, nikiangalia. Nikawaza, “Vema, sasa, ni nini hii?” Unaona? Nao walikuwa wamesimama pale. Nikawaza, “Imekuwaje?” Nikaangalia nyuma kule chini. Ilikuwa ni mimi pale, nimelala pale *pale* chini; tena nilikuwa niko, nimesimama *hapa*. Nikawaza, “Sasa, hilo ni jambo lisilo la kawaida. Si—silielewi.”

365 Na hao wanawake wanapiga makelele, “Loo! ndugu yetu mpendwa,” na kunikumbatia. Sasa, walikuwa katika kila hali, ukiwagusa, ni wanawake.

366 Sasa nisameheni, enyi akina dada, ninaposema jambo hili, maana. . . Lakini msikilizeni daktari wenu; na kama hatuna mawazo safi, basi sisi si Wakristo. Sijali. . .

367 Mimi daima nimeishi maisha masafi. Mungu anajua jambo hilo. Nilipokuwa mvulana mdogo, Malaika wa Bwana aliniambia nisiuchafue mwili wangu, kuvuta sigara, ama kunywa pombe. Na hilo limekuwa ni kweli. Kwa neema ya Mungu, nimetimiza hayo. Nilipokuwa mwenye dhambi, sikutembea na wanawake. Na kwa hiyo. . .

368 Lakini mwanamume ye yote anayemwacha mwanamke amkumbatie kwa mikono yake, yeye akiwa ameumbwa kwa seli za kiume, naye za kike, kuna msisimko. Sijali wewe ni nani, sasa, usiniambie husisimkwi, kama wewe ni mtu mwenye afya timamu.

369 Lakini, si Kule; kwa maana huna, tena, seli tofauti. Hutatenda dhambi Kule kamwe. Kulikuwa na badiliko. Hakukuwako na zaidi ya upendano wa ndugu kwa wanawake hao.

370 Ingawa, katika neema waliyoonekana; ninafikiri, mwa—mwanamke, mwanamke mzuri anayeweka vizuri, na kutembea kama mama wa heshima, yeye ni—yeye ni mfano wa lulu duniani. Mi—mimi napenda kitu cho chote ambacho ni cha madaha. Nafikiri, mwa—mwanamke anayeshikilia mahali pake, na kujitahidi kuwa mama wa kuheshimika, ni—ni mfano wa heshima. Ninaamini hivyo. Nami nafikiri, yule asiye hivyo, ni kama tu Kri—Kristo na mpinga-Kristo, jambo lile lile.

371 Na—napenda kitu cho chote ambacho ni cha asili. Kama vile farasi mzuri, ama cho chote kile, anasimama tu katika umbo lake la farasi mzuri kweli. Ama, kitu cho chote kama hicho, mlima mzuri, wanawake wazuri, wanaume wazuri, cho chote kinachosimama kama kilivyoubwa na Mungu, daima nimekipenda.

372 Na hawa walikuwa ni wakamilifu. Lakini haidhuru wangenikumbatiaje kwa mikono yao, nao walikuwa ni wanawake, mnaelewa, lakini kusingeweza kuwe na dhambi kamwe. Zile tezi za kiume na tezi za kike, zote mbili, zilikuwa zimeondolewa. [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.] Bwana ashukuriwe! Wao walikuwa ni dada zangu, kabisa.

373 Nikaangalia. Nami nikaanza...Ni—nikaangalia mikono yangu; nikaona yote ilikuwa ni michanga sana. Kisha nikaangalia; nilikuwa mchanga, pia. Nami. . .

374 Nami nikiwa nimepoteza nywele zangu, nilipokuwa kijana; kuzitia asidi kabonia, kinyozi alizitia, na kuzing'oa zote nilipokuwa tu mvulana mdogo. Na daima imekuwa kwa namna fulani ja—jambo fulani kwangu, kwamba mi—mi—mimi hupata mafua upesi sana, kwa maana ngozi ya kichwa changu ingali ni nyororo, mwajua. Na mizizi ya nywele ingali iko pale, lakini iliunguzwa na asidi kabonia, na hizo nywele haziwezi kukua kamwe, unaona.

375 Nami nilienda, mke wangu, wakati ni-. . .miaka mingi iliyopita, akaninunulia wigi ya kuvaa, wigi ndogo, ya kuvaa, kufunika kichwa changu. Lakini daima niliona aibu kuvaa, kwa maana ilionekana kama kwamba ni kitu cha bandia. Nami sikutaka kitu cho chote cha bandia.

376 Na kwa hiyo nikawaza, “Nitavaa tu kofia ndogo.” Ndipo, nikaivaa, kwa muda kidogo. Unajua walifanya nini? Walitaka kuniita “askofu” basi, wakasema nilitaka kuwa nanii. . . Mnaona? Nikasema tu, “Na ipotelee mbali.”

377 Kwa hiyo ninateseka sana na mafua makali, na kuiacha ininii. . .Lakini, sasa, mkiyapandisha juu tu madirisha hayo, ama cho chote kile, hewa hiyo kidogo ikija namna hiyo, jamani, nimeyapata tayari.

378 Ndipo nikamwendea daktari na kumwuliza, alifikiria nini. Akasema, “Vema, unaona, vinyweleo vya—vyako viko wazi. Unatoka jasho, kutokana na kuhubiri. Hewa hiyo inakuja. Ina—inaweka kijidudu cha mafua hapa juu kwenye makamasi, nacho kinatolemkia kooni mwako. Asubuhi yake umepwelewa na sauti. Hivyo ndivyo inavyokuwa.”

379 Na—na kwa hiyo, loo! jamani, ninyi watu mlio na nywele, hamjui jinsi inavyowapasa kuwa na shukrani, na kwa kuwa nazo. Hiyo ni kweli. Mnaona?

380 Vema, sasa, niligundua, basi, ya kwamba mimi—mimi nitaninii. . .Moja ya siku hizi, kama nisipopata meno yangu, itanilazimu kupata baadhi yake, na, kwa hiyo, ama kukaa bila meno.

381 Kwa hiyo kama jamaa fulani—kama jamaa fulani. . .Vema, nisingefikiri ingekuwa zaidi kwa mwanamume, kama alitaka kufanya jambo hilo, kuvaa wigi, kuliko vile ingalikuwa kwa mwanamke kuvaa hivi vipanya ama panya, cho chote kile wanachoweka kweye nywele zao namna hiyo, kufanya ubembe. Mnaona? Lakini—lakini, bila shaka, kama ukifanya jambo hilo, inategemea unafanya hivyo kwa sababu gani. Unaona? Inategemea sababu ya kufanya jambo hilo. Na kwa hiyo. . .

382 Lakini, hata hivyo, nikiwa nimesimama pale, nilijigusa juu, nami nilikuwa na nywele zangu tena. Jamani! nilikuwa kijana. Na hawa, hawa wote, vijana! Nami nikawazia, “Vema, si ni ajabu hii! Hawa hapa.” Nao wote walikuwa wanakimbia. . .

383 Nami nikaona, akija, na ni—nilimwona Hope akija. Alionekana. . . Mwajua, yeye alikufa akiwa na umri wa miaka ishirini na miwili. Alikuwa angali ni mrembo tu kama alivyopata kuwa. Wengi wenu mnamkumbuka; hayo macho makubwa meusi. Alikuwa Mjerumani. Nywele zake nyeusi zikining’inia mgongoni mwake. Nikawaza, “Sasa, atakapofika hapa, yeye atasema—atasema, ‘Bill.’ Ninajua atasema hivyo. Ninajua atasema, ‘Bill,’ atakapofika hapa.”

384 Nilikuwa nikiangalia. Na kila mmoja wa wanawake hawa akija akanikumbatia, akisema, “Loo! ndugu mpendwa, tunafurahi mno kukuona!” Nikawazia. . . Kila mmoja amevalia vile vile tu, lakini nywele zao zilikuwa tofauti, unajua, nywele nyekundu, na nywele nyeusi, na nywele za shaba. Nao—nao walikuwa wanakuja, lakini wote walikuwa ni vijana wasichana.

385 Na wakati aliponifikia, nikawaza, “Nitaenda kuona atakalosema.”

386 Ndipo akaniangalia, na kusema, “Loo! ndugu yetu mpendwa! Akanikumbatia, na akaondoka akaenda zake. Mwanawake mwingine akaja, akanikumbatia, anayefuatia.

387 Ndipo nikasikia kelele. Nami nikaangalia upande *huu*, na hili hapa linakuja kundi la wanaume, vijana, wote wakiwa katika umri wa miaka kama ishirini. Walikuwa na nywele nyeusi, na nywele za shaba. Na wote walikuwa na nguo ndefu nyeupe, na hawana viatu. Nao wakanikimbilia na kuanza kunikumbatia, wakipaza sauti, “Ndugu mpendwa!”

388 Nikawaza. Kisha nikageuka kuangalia nyuma, nami nilikuwa niko pale, ningali nimelala pale. Kisha nikawaza, “Vema, sasa, maajabu haya.”

389 Na mara hiyo Sauti ikaanza kunena nami. Sikuiona kamwe Sauti hiyo. Ilisema, “Umekusanywa, u—umekusanywa kwa watu wako.” Na ndipo mwanamume fulani akanichukua, akaniketisha mahali pa juu, kwenye kitu kikubwa na kirefu *hivi*.

Nikasema, “Mbona umefanya hivyo?”

Kasema, “Duniani ulikuwa kiongozi.”

Nami nikasema, “Vema, si—sielewi na jambo hili.”

390 Na Sauti hiyo inanena nami. Sikuweza kuona Sauti hiyo kamwe. Sasa, ilikuwa tu juu yangu, ikinena nami.

391 Nikasema, “Vema, kama ni—kama nimekwisha kuvuka, ninataka kumwona Yesu.” Nikasema, “Mimi. . . Yeye alikuwa ninii sana. . . Alikuwa maisha yangu yote. Ninataka kumwona Yeye.”

Na kwa hiyo, Yeye akasema, “Huwezi kumwona sasa. Yeye angali yuko juu zaidi.”

³⁹² Unaona, ilikuwa chini ya madhahabu, bado, unaona, mahali pa sita, mahali watu wanapokwenda, unaona; si pa saba, mahali Mungu alipo, kiwango cha saba. Cha sita!

³⁹³ Na wao walikuwa—nao wote walikuwa kule, nao walikuwa wanapita. Ndipo nikasema... Ilionekana kana kwamba kulikuwa na mamilioni wao. Sikuwaona hata kidogo... Na, nilipoketi pale, wanawake hawa na wanaume wangali wanakimbia pale na kunikumbatia, wakiniita “ndugu.” Nami nimeketi pale.

³⁹⁴ Na ndipo ile sauti ikasema, “Umekusanywa kwa watu wako, kama vile Yakobo alivyokusanywa kwa watu wake.”

Nikasema, “Watu wote hawa, ati ni watu wangu? Wote hawa ni ukoo wa Branham?”

Akasema, “La. Hao ni waongofu wako kwa Kristo.”

³⁹⁵ Nikaangalia kila upande. Na palikuwapo na mwanamke mwenye sura nzuri sana akanikimbilia. Alionekana karibu tu kama wale wengine. Akanikumbatia, na kusema, “Loo! ndugu yangu mpendwa!” Akaniangalia.

³⁹⁶ Nikawazia, “Jamani! Yeye alionekana kama Malaika.” Kisha akapita.

Ndipo ile Sauti ikasema, “Hukumtambua?”

Nikasema, “La, sikumtambua.”

³⁹⁷ Kasema, “Ulimwongoza kwa Kristo alipokuwa amepita umri wa miaka tisini.” Kasema, “Unajua ni kwa nini anakupenda sana hivi?”

Nikasema, “Ati huyo msichana mrembo alikuwa amepita umri wa miaka tisini?”

³⁹⁸ “Naam.” Ikasema, “Yeye hawezi kubadilika tena sasa.” Ikasema, “Hiyo ndiyo sababu yeye anasema, ‘Ndugu mpendwa.’”

³⁹⁹ Nikawaza, “Loo! jamani! Nami ati niliogopa jambo hili? Mbona, watu hawa wako halisi.” Wao, wao hawakuwa wanaenda mahali po pote. Hawakuchoka, kuwapo Mahali pale.

Ndipo nikasema, “Vema, kwa nini siwezi kumwona Yesu?”

⁴⁰⁰ Ikasema, Vema, sasa, Yeye ataninii—Yeye atakuja siku moja. Naye atakuja kwako, kwanza, na ndipo utahukumiwa.” Ikasema, “Watu hawa ni waongofu wako ambao umewaongoza.”

⁴⁰¹ Nami nikasema, “Unamaanisha, mimi kuwa kiongozi, ni kwamba mimi . . . ni kwamba atanihukumu mimi?”

Ikasema, “Ndiyo.”

⁴⁰² Ndipo nikasema, “Je! kila kiongozi atapaswa kuhukumiwa namna hiyo?”

Ikasema, “Ndiyo.”

Nikasema, “Na Paulo je?”

Akasema, “Itambidi kuhukumiwa pamoja na lake.”

⁴⁰³ “Vema,” nikasema, “kama kundi lake likiingia, na langu pia, maana nimehubiri Neno lile lile kabisa.” Ndio hivyo. Nikasema, “Pale alipobatiza katika Jina la Yesu, na mimi pia, nilibatiza. Nilihubiri. . .”

⁴⁰⁴ Na mamiloni wakapaza sauti, wote mara moja, wakasema, “Tunategemea jambo Hilo!”

⁴⁰⁵ Nami nikawazia, “Jamani! Laiti ningalijua tu jambo hili kabla ya kuja mahali hapa, ningewafanya watu waje hapa. Hawawezi kuthubutu kukosa kitu hiki. Mbona, hebu angalia hapa!” Halafu basi. . .

⁴⁰⁶ Naye akasema, “Sasa, siku moja Yeye atakuja, na ndipo. . . Sasa, ndani hapa, hatuli, hatunywi, wala hatulali. Sote ni mmoja tu.”

⁴⁰⁷ Vema, si pakamilifu; ni zaidi ya kukamilika. Si pa heri, ni zaidi ya heri. Hakuna jina linaloweza. . .Huwezi kuwazia. . . Hakuna maneno katika msamiati ya kuitamka hali hiyo. Umewasili tu, basi.

⁴⁰⁸ Nami nikawazia, “Vema, hii, hii ingekuwa kamilifu. Na basi tutafanya nini tena?”

⁴⁰⁹ Kasema, “Halafu, Yesu atakapokuja, nasi tunaninii. . . Naye anakuhukumu, ama kwa ajili ya huduma yako, basi tutarudi duniani na kuchukua miili.” Vema, si—sikuwazia jambo hilo wakati huo. Hilo ni Maandiko kabisa. Wakasema, “Ndipo tutarudi duniani na kuchukua miili, ndipo tutakula. Hatuli hapa, wala hatulali.” Wakasema, “Tunakula kule chini, lakini tunarudi duniani.”

⁴¹⁰ Nikawazia, “Jamani, hilo si ni la ajabu! Loo! jamani! Nami nilikuwa ninaogopa jambo hilo. Kwa nini nilikuwa nikihofu kufa, nipate kuja kwenye hali hii? Vema, huu ni ukamilifu, kuongeza ukamilifu, kuongeza ukamilifu. Loo! ni jabu la kustaajabisha sana!”

⁴¹¹ Unaona, tulikuwa hasa chini ya madhabahu. Unaona? Hivyo ndivyo ilivyokuwa, unaona, hasa chini ya madhabahu, tusingojea kule Kuja, unaona, ili Yeye aende akawachukue wale waliokuwa wamelala katika. . .mi—miili inayolala mavumbini, kutufufua tena; aje, atufufue.

⁴¹² Kama vile Yesu alivyopitia paradiso, na akamfufua Ibrahimu, Isaka, na hao wote, unajua, waliokuwa wanangojea ule ufufuo wa kwanza. Wao waliingia mjini na kuwatokea wengi.

⁴¹³ Ni la Kimaandiko kabisa. Lile ono lilikuwa hivyo, ama cho chote lilivyokuwa, lilikuwa ni la Kimaandiko kabisa.

414 Nami nikasema, “Vema, si ni ajabu hii!” Na ndipo nikawazia, “Hilo si ni aja- . . . ?”

415 Nikasikia kitu fulani kikilia kwa utulivu, kama farasi. Ndipo nikaangalia. Na maskini farasi wangu wa kusafiria niliyekuwa nikimpanda, maskini Prince, nilimpenda sana. Huyu hapa, amesimama pale karibu nami, naye akakiweka kichwa chake kwenye bega langu, kunikumbatia. Kama vile nilivyozea kumpa sukari, unajua, naye akaweka ninii yake. . . Nikamkumbatia kwa mkono wangu. Nikasema, “Prince, nilijua ungekuwa hapa.”

Nikasikia kitu fulani kikiulamba mkono wangu. Huyu hapo maskini mbwa wangu wa kuwinda.

416 Wakati—wakati Bw. Short, hapa, alipompa sumu, niliapa nitamwua Bw. Short kwa ajili ya jambo hilo. Nilikuwa na umri wa miaka kama kumi na sita. Alimpa sumu, akampa chakula cha kuua mbwa. Na baba yangu akanikuta na bunduki, nikishuka kwenda kumpiga risasi, moja kwa moja kwenye kituo cha polisi. Nami nikasema, “Nitamwua.” Nikasema, “Vema. . .” Nikaenda kwenye kaburi la mbwa huyo. Na nikamwambia, nikasema, “Fritz, umekuwa kama rafiki kwangu. Umenivika nguo na kunipeleka shuleni. Ulipokuwa mzee, ningekutunza. Sasa wamekuua.” Nikasema, “Ninakuahidi, Fritz, ya kwamba yeye hataishi.” Nikasema, “Ninakuahidi, yeye hataishi. Pana siku nitampata mitaani, akitembea, ndipo nitamkanyaga kwa gari, unaona.” Kisha nikasema, “Nitakulipizia kisasi.”

417 Lakini unajua nini? Nilimwongoza mtu huyo kwa Kristo, nikambatiza katika Jina la Yesu, na nikamzika alipokufa. Ndiyo, bwana. Niliongoka yapata miaka miwili baada ya jambo hilo. Niliona mambo tofauti wakati huo, unaona. Nilimpenda badala ya kumchukia.

418 Kwa hiyo basi, lakini, hata hivyo, huyo hapo Fritz alikuwa amesimama pale, akinilamba mkononi. Nami nilikuwa. . . nikaangalia.

419 Nisingeweza kulia. Hakuna mtu angaliweza kulia. Ilikuwa ni furaha tupu. Hungeweza kuwa na huzuni, maana ilikuwa ni furaha tupu. Hungeweza kufa, maana yote ilikuwa ni Uzima mtupu. Unaona? Unaona? Hungeweza kuwa mzee, maana ilikuwa ni ujana mtupu. Na hiyo ndiyo. . . Ni kamilifu tu. Niliwazia, “Loo! hili si ni jambo la kustaajibisha sana!” Na hao mamilioni. . . Loo! jamani! Nilikuwa nyumbani kabisa, unaona.

420 Na—na mara nikasikia Sauti. Nayu ikalia, ikasema, “Vyote ulivyowahi kupenda. . .” thawabu ya huduma yangu. Sihitaji thawabu yo yote. Akasema, “Vyote ulivyowahi kupenda, na wote waliowahi kukupenda, Mungu amekupa.”

Nikasema, “Bwana na asifiwe!”

421 Nikajisikia wa ajabu-ajabu. Nikawazia, “Kuna nini? Ninajisikia wa ajabu-ajabu.” Nikageuka na kutazama. Na kule juu ya kitanda, mwili wangu ulikuwa ukitikisika. Nikasema, “Jamani! kweli, sitalazimika kurudi, kweli. Usininii, usinirudishe.”

422 Lakini Injili ilipaswa kuhubiriwa. Katika sekunde moja tu, nilikuwa niko kitandani tena, unaona, namna hiyo.

423 Si zaidi ya miezi miwili iliyopita, ambapo... Mlilisikia likisomwa kwenye—kweye gazeti la *Sauti* ya Wafanyi Biashara. Lilisambazwa ulimwengu mzima, mnaona. Naye Ndugu Norman, aliye hapa, ninadhani yuko hapa mahali fulani usiku wa leo. Yeye aliitafsiri kutoka kwenye hilo, na kulisambaza katika vitini. Limeenda kila mahali. Nao wahudumu wakaandika, wengi wao, na kusema...

424 Mmoja hapa, nitasimulia tu hili hapa. Kumekuwa na mamia yao, bila shaka. Huyu alikimbia, akasema, “Ndugu Branham, ono lako kwenye gazeti la *Sauti* ya Wafanyi Biashara...”

425 Nami ninampenda Tommy Nickels, ingawa yeye hayuko pamoja na Wafanyi Biashara, tena. Sijui ni kwa nini, bali hayuko pamoja nao. Lakini yeye aliliweka pale sawa kabisa, ambapo nilisema. Pale pale kwenye gazeti hilo la wanaoamini utatu, akasema, “Pale ambapo... Pale Paulo alipobatiza katika Jina la Yesu, na kuwaamuru watu kufanya jambo lile lile, nimefanya vivyo hivyo.” Unaona, yeye aliliweka jinsi tu lilivyokuwa. Unaona? Na halafu basi ni—ni—nikawazia, “Jamani!”

426 Mhudumu huyu aliniandikia, akasema, “Ndugu Branham, ono lako...”

427 Ambalo, lingeweza kuwa ni ono. Kasema... Sasa, mimi sitaki kusema, “kuhamishwa.” Kama Paulo... Kama nilikuwa nimenyakuliwa mpaka mbingu hii ya kwanza na kuona jambo hilo, vipi kuhusu Paulo! aliyenyakuliwa mpaka kwenye mbingu za tatu? Hiyo ilikuwa ni nini? Yeye alisema hata hangeweza kunena habari zake, unaona, kama alinyakuliwa. Kama ilikuwa ni kunyakuliwa, sijui. Siwezi kusema. Singeweza kuwaambieni.

428 Lakini mhudumu huyu alisema, “Ndugu Branham, ono lako lilisikika la Kimaandiko sana na la kweli mpaka ulipozungumzia juu ya kuwako kwa farasi kule.” Kasema, “Ati farasi Mbinguni?” Kasema... Sasa unamwona mtu huyo wa kidini, hekima, bongo? Unaona? Akasema, “Mbingu iliumbwa kwa ajili ya wanadamu, si farasi.”

429 Vema, nikaketi. Billy, mwanangu hapa, akaiweka ile barua papa hapa katika ofisi ya kanisa la zamani, yapata miezi mitatu ama minne iliyopita.

430 Nikasema, “Ndugu yangu mpendwa, ninashangazwa na hekima yako, lakini, na ujuzi wako wa Maandiko. Sikusema ya kwamba nilikuwa Mbinguni. Nilisema ilikuwa ni mahali

kama paradiso, maana Kristo alikuwa angali yuko juu, unaona. Lakini,” nikasema, “kama linaweza kukuridhisha, fungua Ufunuo 19. Na wakati Yesu atakapotokea kutoka kwenye mbingu za Mbinguni, Yeye atakuwa amepanda farasi mweupe, na watakatifu wote pamoja Naye wamepanda farasi mweupe.” Hakika. Kweli kabisa. Naam, hakika.

431 Na pale kwenye Mahali pale pale, kulikuwako na mmoja aliyeonekana kama tai, na mmoja aliyeonekana kama ndama, na mmoja. . . Vema, jamani, wale farasi waliokuja kumchukua Eliya wako wapi? Inaonyesha tu, unaona, ya kwamba akili ya mwanadamu inataka tu jambo la kubishania. Hiyo ni kweli.

432 Sasa angalia. Lakini nilikuwa nikiwazia tu, kama huyu ndugu wa thamani na mcha Mungu, Yohana. . . Nilifikiri tu pangukuwa ni mahali pazuri pa kuingizia jambo hilo, kabla tu ya kufunga, unaona. Kama Yohana aliangalia Kule, na hao walikuwa ni baadhi ya ndugu zake, unaona, ndugu zake ambao walipaswa kuteswa muda kidogo; basi, unaona, Bwana Mungu aliniruhusu kuwaona ndugu zangu na watakatifu waliokuwa wanakungojea kule Kuja kwa Bwana. Angalia, wao hawakuwa chini ya madhabahu ya dhabihu; wangu hawakuwa pale. Lakini, hawa walikuwa kule, walikuwa ni wafia imani. Unaona? Wangu hawakuwa chini ya madhabahu ya wafia imani.

433 Sasa nawatakeni msikilize kwa makini sana. Nami nitafunga, kweli, katika muda wa dakika kama kumi hivi, saa nne, kama itanibidi kuukatisha tu na kuumalizia kesho.

434 Angalieni. Wao, wao hawakuwa ninii wangu. . . wale ambao Bwana alinionyesha, Bibi-arusi, Yeye hakuwa chini ya madhabahu ya wafia imani, la, madhabahu ya dhabihu ya wafia imani; lakini walikuwa wamepokea nguo ndefu nyeupe, kwa kukubali neema yenye kusamehe ya Neno lililo hai. Kristo alikuwa amewapa nguo ndefu nyeupe. Sidhani, kwa kufunguliwa. . .

435 Ama, ninafikiri, hasa, kwa kufunguliwa kwa Muhuri huu wa Tano, kama ninavyoamini, ya kwamba umefunguliwa kwetu. Nilifanya jambo hilo nikiwa na dhamiri njema, nikiwa na ufunuo dhahiri mbele za Mungu. Si kujaribu tu kujifanya, kuwazia, kwa sababu daima niliyapinga madhehebu, kamwe nisingekuwa mfuasi wake. Lakini Huo umefunguliwa kwangu sasa.

436 Nami ninafikiria jambo lingine. Kwa kufunguliwa kwa Muhuri huu wa Tano, katika siku hii, kunanyosha fundisho fulani papa hapa, ambalo huenda nikazungumza habari zake, la kulala kwa nafsi. Sasa, ninatambua ya kwamba kuna watu hapa ndani wanaoamini hilo, unaona, katika kulala kwa nafsi. Nafikiri Huo unakanusha hilo. Wao hawakulala. Wako hai. Miili yao, imelala. Lakini, nafsi, haiko kaburini, wao wako katika Uwepo wa Mungu, unaona, chini ya madhabahu.

437 Hapa ndipo ninapohitilafiana na ndugu mmoja mpendwa, mwalimu mmoja. Na, ninaona, ninajua ninawaona baadhi ya watu wake wameketi hapa. Kwamba, ninatambua ya kwamba huyu ni mwalimu mkuu. Yeye ni daktari, na ni Da—Daktari wa Uungu, na ana Ph., LL.D.. Naye ni m—mtu mzuri kweli, pia. Nafikiri amesha aga dunia, wakati huu. Lakini yeye alikuwa mtu mzuri, na mwandishi mzuri. Naye ni Ndugu Uriah Smith, mwandishi wa kitabu kiitwacho *Danieli na Ufunuo*. Sasa, kwenu ninyi watu mlio wafuasi wa mafundisho yake, mnaona, sasa mimi sininii . . . Mimi sininii tu . . . sitaki kusema jambo hili kwa majivuno, lakini mimi ninaninii tu . . . Mnaona?

438 Lakini, Ndugu Smith, na kujaribu kuunga mkono, unaona, na kujitahidi kuunga mkono kulala kwa nafsi, hapo analitaja jambo hilo, “Nafsi hulala. Na hakuna madhabahu ya dhabihu Mbinguni. Ni hivi kwamba, madhabahu pekee inayonenwa ni,” ambayo yeye—yeye anaamini iko Mbinguni, “ni madhabahu ya uvumba.” Lakini kwenu ninyi watu wapendwa . . . Na sio kwamba ninakataa kuchukuliana na ndugu yangu. Labda mimi . . . ninatumaini nitakutana naye ng’ambo ya pili, unaona. Sio kwamba ninahitilafiana na huyo mwalimu mkuu.

439 Lakini ni kuwaonyesha tu jinsi Huu unavyokanusha jambo hilo, mnaona. Unalikanusha. Kufunguliwa kwa Muhuri huu katika siku hii ya mwisho, kunaondolea mbali kulala kwa nafsi moja kwa moja. Unaona? Wao wako hai. Hawakufa. Unaona? Angalia.

440 Angalia jambo hili sasa. Sasa, kama hakuna madhabahu ya dhabihu Mbinguni, dhabihu ya dhambi imewekwa wapi basi, yule Mwana-Kondoo? Hapana budi kuwe kuna mahali ambapo yule Mwana-Kondoo aliyechinjwa, aliyejaa damu, amekaa pale, ambapo ile Damu . . . ninii.

441 Sasa, ule uvumba ulikuwa ni zile harufu nzuri, vile vitu vyenye harufu nzuri walivyoteketeza, ambavyo Biblia ilisema ilikuwa ni “maombi ya watakatifu.” Kama hakuna dhabihu kwenye madhabahu, basi maombi hayawezi kupokelewa. Ni kwa Damu tu, kwenye madhabahu ya dhabihu, inayowezesha maombi yamwendee Mungu.

442 Ndugu Smith alikosea, unaona. Si kwamba sitaki kukubaliana naye; ninadhani nilijieleza wazi, kwa upendano wa ndugu na heshima kwa ajili ya kazi yake kuu, mnaona. Lakini alikuwa amekosea.

443 Muhuri wa Tano umelifungua jambo hilo, unaona, unaona; mambo mengine mengi, kama mliupata. Unaona? Ninangojeka maswali yangu, mnaona, kama mimi . . . Vema.

444 Sasa, lile sanduku la agano lilikuwa wapi; Mwana-Kondoo aliyechinjwa, aliyejeruhiwa, anayetoka damu, na aliyejaa damu kwa upatanisho, kwa ajili ya maombi haya yenye harufu nzuri?

445 Angalia, Biblia inasema, “Kama maskani hii iliyo ya dunia hii ya makazi yetu tunayoishi ikiharibiwa, tunayo nyingine inayongojea tayari.” Huko ndiko nilikowaona hao watakatifu. Mnaona?

446 Angalia wakati mtoto mchanga... Samahani tena, akina dada, kwa ajili ya mazungumzo haya ya waziwazi mbele ya vijana wanawake. Lakini, angalieni. Wakati mama amechukua mimba, na hilo bongedogo la misuli linachezacheza na kurukaruka, mnaelewa, ni mwili wa kawaida. Na kama tu vile maumbile yanavyofanya kwa mwili wa kawaida...

447 Je! ulipata kuchunguza mkeo kabla ya mtoto kuzaliwa? Yeye daima, wakati wote, wakati wa mwisho, anakuwa mwema sana, mtu mzuri. Kama hajawahi kuwa, hiyo maishani mwake mwote, basi atakuwa hivyo wakati huo. Ulipata kuona jinsi alivyo wa kitawatawa sana, ama kuwa na hali ya kuwa mwema, umemchunguza huyo mama?

448 Na unaona mwenye dhambi fulani huko nje, wakimfanyia mzaha mama ambaye ni mwanamke m—mja mzito. Ninafikiri huo ni upuuzi. Huo ni uhai unaokuja duniani.

449 Lakini uliwahi kuona, kwa huyo mama kuna kuonekana kwa hali ya upole aliyo nayo? Ni kitu gani? Ni mwili mdogo wa kiroho, uhai wa kiroho, ukingojea kuja kwenye mwili huo mdogo mara tu utakapozaliwa. Kwa sasa ameshika mimba tu; lakini, wakati atakapozaliwa, amezaliwa. Mwili huo wa kiroho unaungana na mwili wa kawaida.

450 Na, halafu, basi, Biblia inafundisha ya kwamba sisi sasa tumetunga mimba ya Mungu. Tumetunga mimba ya Roho Mtakatifu, ya kwamba, ndani yetu yumo Kristo, mwana wa Mungu akiumbika ndani yetu. Na wakati mwili huu ulio wa dunia hii utakapoharibiwa, mwili huu wa kiroho unapokuja kutoka kwenye moyo wa nchi, kuna mwili mwingine unaungoza kuupokea. “Maskani hii iliyo ya dunia hii ikidondoshwa, tunalo jengo lingine la kuipokea.” Mwili huu unaopatikana na mauti unavaa kutokuharibika. Huu wa duniani unavaa wa kimbinguni. Huu, mnaona ninalomaanisha? Kuna mwili wa kawaida ambao ni wa dhambi; lakini, katika kufanywa kwake, ni kama huo tu, kuna mwili mwingine tunaouendea.

451 Nami ninamshukuru sana Mungu kwamba ninaweza kusema, kama mchungaji wenu na ndugu yetu, nimewaona watu hao, kwa hiyo anisaidie, katika mwili huo, na niliwashika kwa mikono yangu. Hiyoni kweli. Angalia.

452 Angalia. Waangalie Musa, Elisha. Baada ya Musa kufa, na Elisha amekwisha kuchukuliwa Mbinguni, yeye alisimama hapa kwenye Mlima wa Kugeuzwa Sura akiwa na hisi zake za kuzungumza, kusikia, kufahamu, na wakazungumza na Yesu kabla ya kule kusulubishwa. Sasa, yeye alikuwa na mwili wa namna gani?

453 Mwangalie Samweli, baada ya kufa kwa miaka kama miwili. Aliitwa arudi pa—pangoni usiku ule, na yule mchawi wa Endori, na akazungumza na Sauli katika lugha; akamsikia Sauli, akamjibu, na alitangulia kujua mambo ambayo yangetukia. Hata hivyo, roho yake haikuwa imebadilika. Yeye alikuwa ni nabii.

454 Wakati roho ya Eliya itakapokuja juu ya mtu huyu, itamwongoza kama tu Eliya. Yeye ataenda nyikani. Atapenda nyika. Atakuwa mchukia wanawake wazinzi. Atayapinga madhehebu. Hatacheza na mtu ye yote. Na hilo ni ninii tu. . . Hiyo ni, hiyo itakuwa ni roho yake. Ilikuwa hivyo, kila wakati ilipokuja, unaona.

Musa atakuwa ni mtu yule yule.

Sasa, nasi tunaona, katika Ufunuo 22:8, jambo lile lile.

455 Sasa, ama kulitatua, kwa ajili ya wale ambao. . . Roho zile (sasa angalieni jambo hili) chini ya madhabahu, kwa kuvunjwa kwa Muhuri hii, ambao walikuwa wameuawa kati ya kifo cha Kristo na kunyakuliwa kwa Kanisa; lile kundi la Eichmann, na hao wote, hao Wayahudi wa kweli walioandikwa majina yao katika kile Kitabu. Kama utaangalia vizuri, ndugu yangu, kulingana na Maandiko, wao waliweza kuzungumza, kupaza sauti, kuongea, kusikia, nao walikuwa na zile hisi zote tano. Si kulala kaburini, wakiwa hawana fahamu. Walikuwa wako macho sana, nao wangeweza kuzungumza, kuongea, kusikia, kitu cho chote kile. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Jaman, tusaidie!

456 Dakika mbili. Amina. Samahani niliwachelewesha nusu saa. La, siwezi, sipaswi kusema jambo hilo, unaona. Unaona? Hiyo ni kweli, unaona.

457 Lakini, angalieni, hivi ndivyo jinsi ninavyofahamu mimi kwa uwezo wangu wote, uwezo wangu wote. Na kulingana na ufunuo niliopewa asubuhi ya leo kabla tu ya mapambazuko, na Bwana Yesu Kristo, huo hapo Muhuri wa Tano uliofunguliwa, kuambatana na ile mingine minne. Kwa neema Yake, Yeye aliunipa mimi, neema Yake kwa ajili yenu na kwa ajili yangu. Tunamshukuru kwa ajili ya jambo Hilo. Na, pamoja na msaada Wake, ninatarajia kuishi karibu zaidi. . . niwezavyo kuishi, nikiwafundisha wengine kufanya jambo lile lile, mpaka nitakapomlaka Yeye, pamoja na ninyi, Utukufuni, wakati mambo yote yamekwisha. Ninapenda kwa ajili ya jambo hili, na kwa uwezo wangu wote nijuavyo mimi juu ya jambo Hilo.

458 Nami ninaamini kweli, kwa moyo wangu wote, ya kwamba mafunuo ya kweli ya kufunuliwa kwa Muhuri wa Kwanza, wa Pili, wa Tatu, wa Nne, na wa Tano, sasa yamefunguliwa kwetu.

Nampenda, nampenda

Kwani alinipenda kwanza

[Ndugu Branham anazungumza pole pole na mtu fulani—Mh.]

Mtini Kalvari.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.]

⁴⁵⁹ Sasa, pole pole, kwa uchaji, mbele za Mungu! Kama tulivyoona Muhuri huu umefunguliwa kwetu, ilibidi Mungu kuwachukuwa watoto Wake Mwenyewe wapendwa na kuyapofusha macho yao, na kuwafukuzia mbali, kwa maana haki Yake Mwenyewe—haki inahitaji hukumu ya dhambi. Wazia jambo hilo. Haki Yake, na utakatifu Wake unahitaji haki. Sheria isiyo na hukumu si sheria. Na sheria Zake Mwenyewe, Yeye Mwenyewe, hawezi kuziasi na bado abakie kuwa Mungu.

⁴⁶⁰ Hiyo ndiyo sababu ilimbidi Mungu kufanyika mwanadamu. Yeye hangechukua kibadala, mwana ambaye hakuwa . . . mwana wa kawaida tu Kwake, ama cho chote kile. Mungu alifanyika wote wawili, Yesu alifanyika Mwana na Mungu pia, njia pekee ambayo angaliweza kufanya jambo hilo kwa haki. Ilimbidi Mungu abebe adhabu, Yeye Mwenyewe. Haingekuwa haki, kuiweka juu ya mtu mwingine, mtu mwingine. Kwa hiyo, Utu wa Yesu ulikuwa ni Mungu, aliyedhihirishwa katika mwili, ulioitwa Imanueli.

⁴⁶¹ Na ili kufanya jambo hilo, na kumchukua Bibi-arusi, na kuokoa kundi lililopotea la makafiri wa Mataifa, ilimbidi Yeye kuwapofusha watoto Wake Mwenyewe. Halafu awaadhibu kwa ajili ya jambo hilo, katika mwili, kwa ajili ya kumkataa. Lakini neema yake iliwapa nguo ndefu. Lakini, ule Uzima, angalia yaliyotukia.

⁴⁶² Na kama ilimbidi Yeye kufanya jambo hilo, ili kwamba sisi tupate nafasi, tunawezaje kupuuza nafasi hiyo katika upendo? Kama kuna mtu katika jengo hili, usiku wa leo, mtu huyo, kijana au mzee, ambaye mpaka wakati huu ameisukumia mbali nafasi hiyo iliyomgharimu Mungu gharama kama hiyo, nawe ungetaka kukubali nafasi hiyo kwa Mungu, usiku wa leo; ya kwamba si lazima, kadiri tujuavyo sisi, kuwa mfia imani, ingawa unaweza kuwa. Lakini nguo ndefu nyeupe imetolewa kwa ajili yako. Na kama Mungu anagonga moyoni mwako sasa, kwa nini usikubali jambo hilo! [Ndugu Branham aligonga mimbara mara tatu—Mh.]

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu tena.

⁴⁶³ Kama mtu huyo, ama watu, wako humu ndani, ambao wanataka jambo hilo, ama wanataka kulikubali juu ya msingi wa imani yako katika Damu iliyomwagika ambayo ilimbidi Mungu kumwaga kwa ajili yako, akateseka zaidi ya cho chote ambacho mwanadamu mwingine ye yote. Kusingeweza kuwa na mwanadamu ambaye angeweza kutesaka namna hiyo. Mpaka, huzuni Yake Mwenyewe iliyatenganisha maji Yake kutoka kwenye Damu Yake, katika mishipa Yake ya Damu. Kabla

hajaenda Kalvari, matone ya Damu yalikitoka kwenye mwili Wake, akiwa na huzuni kubwa sana na moyo uliovunjika juu ya yale yaliyompasa kufanya. Lakini, yeye angeweza kukataa jambo hilo, pia. Lakini, yeye alijitolea kwa ajili yako na kwa ajili yangu. Unaweza kukataa upendo kama huo usio na kifani?

⁴⁶⁴ Nawe sasa unaona hayo, kwa kufunguliwa kwa Mihuri hii; yale uliyofanya, na yale Mungu aliyokufanyia. Nawe uko tayari kumtolea Mungu maisha yako, na kama Yeye atakunyakua kutoka katika mikono ya mpinga-Kristo ambamo umo ndani yake sasa? Je! unaweza kukubali nafasi aliyotoa, kwa kumvunulia tu Yeye mkono wako, ukisema, “Mungu, kwa huu, ninadhihirisha. Ninakubali toleo hilo la neema.”

⁴⁶⁵ “Na, Ndugu Branham, ninataka maombi yako, ya kwamba daima nitadumu mwaminifu.”

⁴⁶⁶ Inua mkono wako, nami nitaomba. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Maanisha hilo sasa. Usi—usifanye jambo hilo isipokuwa unamaanisha. Na papo hapo unapoketi, likubali papo hapo. Maana, kumbuka, usingeweza kuinua mkono wako isipokuwa Kitu Fulani kilikwambia ufanye hivyo. Na hakuna kitu kingine kingeweza kukwambia isipokuwa ni Mungu.

⁴⁶⁷ Kwa hiyo, sasa, wakati unapoona Maandiko yakifunuliwa kikamilifu sana! Unaona yale yaliyokuwa yakiendelea, katika nyakati, miaka michache iliyopita, miaka ishirini ama thelathini. Unaona jambo hilo likithibitishwa kikamilifu. Unaona Maandiko yakisema kile hasa kilichotendeka, na kile kinachokaribia kutendeka. Basi, juu ya msingi wa imani katika kazi Yake Kristo, mahali unapoketi sasa hivi, nawe umeinua mikono yako, sema, “Tangu dakika hii na kuendelea, imekwisha. Ninamchukua Kristo sasa kuwa Mwokozi wangu. Nami nitamwishia Yeye, maisha yangu yote. Nami ninataka Mungu anijaze na Roho Mtakatifu.” Na kama hujabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kidimbwi kitakuwa kikikungojea.

Na tuombe.

⁴⁶⁸ Bwana Mungu, kulikuwako na idadi kubwa ya mikono kati ya watu, iliyoinuliwa. Nina hakika Wewe ni Bwana Yesu yeye yule aliyetufanyia upatanisho, miaka mingi iliyopita. Na kwa kuona Mihuri hiyo imefunuliwa, na mambo yale makuu yaliyotukia papa hapa katika miaka michache iliyopita, ninaamini kwa moyo wangu wote ya kwamba mlango wa neema umeanza kufungwa, Nawe uko tayari kufanya safari Yako sasa kuwakomboa watu Wako. Wakati kuna nafasi, na mlango umefunguliwa, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, naomba nafsi hizi za thamani zinazoishi kwenye mwili wa maskani hii ambayo siku moja itaharibiwa, walioinua mikono hii ipatikanayo na mauti, ndani yao; kwa sababu ya—ya kuguswa kwao na kukiri kwao, ya kwamba wanaamini na wanataka kukubali azimio Lako kwao, kwa ajili ya wokovu,

kwenye Kitabu hiki kilicho wazi kilichotiwa muhuri ambacho kimefunguliwa kwetu. Wape, usiku wa leo, Bwana, nguo ndefu za haki ya Yesu Kristo, na uvalishe nafsi yao katika hiyo, ili waweze kusimama mbele Yako kwenye Siku hiyo ambayo inakaribia, wakiwa wamekamiliwa, kwa Damu ya Kristo.

⁴⁶⁹ Bwana Mungu, kama wao hawajabatizwa katika Jina la Yesu Kristo! Na juu ya ufunuo ambao Wewe ulinipa kuhusu jambo hilo; na kuona kwamba Paulo aliwaamuru watu waliokuwa hata wamebatizwa na Yohana Mbatizaji, kubatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo, kusudi wampokee Roho Mtakatifu, katika Matendo 19. Ninaomba ya kwamba Wewe utawashawishi, Bwana, kuhusu ile Kweli, na naomba wao wakutii Wewe.

⁴⁷⁰ Na halafu katika kutii kwa kukubali kwao, na katika kutii kwa kuungama kwao, na kwenye maji; nakuomba, kwa upande Wako uwajaze na Roho Mtakatifu, kwa ajili ya nguvu za utumishi, maishani mwao mwote. Ninawakabidhi Kwako sasa, katika Jina la Mwana-Kondoo wa Mungu aliyetolewa sadaka, Yesu Kristo. Amina. Amina.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

⁴⁷¹ Sasa, kwenu ninyi mliokuwa mmeinua mikono yenu. Tiini amri ya Roho, ambayo ingefuata ka—katiba ya Neno, kwa ajili ya mwenye dhambi aliyetubu. Ifuateni, katika kila tendo. Na Mungu wa Mbinguni na awajazi kwa ajili ya msimamo wenu Kwake. Bwana awabariki.

⁴⁷² Kesho usiku, leteni penseli zenu na makaratasi, sasa, kama vile mlivyokuwa mkifanya. Tunatarajia kuwa hapa kwenye wakati ule ule, saa moja na nusu, kamili, Bwana akipenda. Na kwa . . . niombeeni, kwamba Mungu atanifungulia Muhuri wa Sita, kesho, ili niweze kuuleta kwenu jinsi anavyounipa mimi. Mpaka wakati huo, tuimbe tena. Si katika nyimbo tu, lakini katika sifa kwa ajili Yake Yeye aliyekufa badala yetu na kutukomboa. *Nampenda*. “Na- . . .

Huyu hapa mchungaji wenu sasa.

. . . mpenda, nampenda

Kwani alinipenda kwanza.



UFUNUO WA MIHURI SABA
(The Revelation Of The Seven Seals)

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham zilihubiriwa kutoka tarehe 17 Machi mpaka tarehe 24 Machi, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, na Muhuri wa Saba ukaendelea tarehe 25 Machi katika Hoteli ya Sherwood. Baada ya kupata kanda za awali ambazo zinasikika vizuri na ni kamilifu zaidi, kitabu hiki kimechapishwa tena kwa mpangilio wa sasa. Kila jitihada imefanywa kuhamisha kwa usahihi Ujumbe wa sauti kutoka kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuuandika katika kitabu, na umechapishwa hapa bila kufupishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

Haki zote zimewekwa. Kitabu hiki hakiwezi kuuzwa, kuchapishwa tena, ama kufasiriwa katika lugha zingine, ama kutumiwa kwa kuchangisha fedha bila barua ya kuruhusia ya William Branham Evangelistic Association. Kilichapishwa tena katika mwaka wa 2006.

SWAHILI

©2001 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org